

SANDA YA YESU

SAFARI YAKE

na

KABURI LAKE

SANDA YA YESU, SAFARI YAKE NA KABURI LAKE

© Ahmadiyya Muslim Jamaat, Tanzania

Chapa ya Kwanza ya Pili: 2009

Nakala: 2000

Kimeenezwa na:

Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya, Tanzania

Mnazi mmoja, Dar es Salam.

Simu: +255222110473

Fax: +255222121744

Kimechapwa na:

Ahmadiyya Printing Press

Dar es Salam. Tanzania

Simu: +255222111031

ISBN 9987 - 438 - 09 - 1

YALIYOMO

NENO LA MBELE	v
UTANGULIZI	vii

MLANGO WA KWANZA:

Sanda ya Yesu	1
Sanda yenyewe	1
Historia ya Sanda	2

MLANGO WA PILI:

Maelezo ya Uvumbuzi wa Mwanzo.....	4
Jambo jingine	4
Swali kubwa.....	5

MLANGO WA TATU:

Maelezo juu ya Uvumbuzi wa Pili	6
Shangwe	7

MLANGO WA NNE:

Maelezo juu ya Uvumbuzi wa Tatuu	10
Muhutasari wa Maoni juu ya Utafiti huo	11
Umaarufu wa Mchoro wa Bwana Rambrandt	12
Magazeti	13
Maandiko ya Yohane	13
Maelezo ya Kurani Tukufu Juu ya Kusulubiwa kwa Yesu na Hatimaye	15
Maoni ya Ahmadiyya kumhusu Yesu	16

MLANGO WA TANO:

Ubishi dhidi ya Sanda na dhidi ya Dalili zake	18
Umri wa Sanda ya Turin	18
Nguo ya zamani kiasi hiki ingewezaje kukaa hata sasa?	19
Je, mawaa yaliyomo Sandani ni rangi iliyopakwa?	20
Uamuzi wetu sisi wenyewe	22
Kutegemeka kwa utafiti	23

MLANGO WA SITA:

Habari zingine kuhusu Sanda	27
Kanisa laainisha Imani Yake	27
Sanda kuchunguzwa na Wataalamu	29
Askofu Mkuu wa Turin ahojiwa redioni	30
Sanda yaonyeshwa katika Televisheni	32

MLANGO WA SABA:

Hatimaye	34
Sanda kufanyiwa majoribio ya ndani	35

MLANGO WA NANE:

Ishara ya Yona	37
----------------------	----

SEHEMU YA PILI:

UVUMBUZI MWINGINE	39
Ugunduzi wa Maandiko ya mwaka A.D. 40 huko Alexandria	40
Marham ya Yesu	44
Kagunduliwa kwa Ushuhuda wa Petro	46
Kugunduliwa kwa Ufupisho wa Kitabu cha Marko	47
Kugunduliwa kwa "Matendo ya Thoma"	49
Yesu huko Taxilla	50
Kaburi la Mt. Thomaso	51
Kugunduliwa kwa maandiko huko Nag Hamad	52
Kugunduliwa kwa Hati za Maandiko karibu ya Bahari ya Chumvi:	54
Hati za maandiko ya Kale zathibitisha mambo matatu	58
Zaburi za Shukrani	59
Ugunduzi kutoka kituo cha Wabudha:	60
Maoni ya Waislamu Waahmadiyya kuhusu Ugunduzi wa Notovitch	63
Ugunduzi kutoka kitabu cha Bhavisha Maha Purana	64
Maandiko yaliyochongwa penye Ukumbusho wa Takhte-Suleiman	66
Ugunduzi wa Kaburi la Yesu	67
Athari ya uvumbuzi huu	72
Ziara, Maoni na Ufafanuzi	73
Kwa nini Kaburi lisifikuliwe?	78
Biashara	79

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwingi wa Ukarimu.

NENO LA MBELE

Kitabu hiki ambacho kiliandikwa kwa Kiingereza kililetwa hapa Nairobi mnamo mwaka wa 1979. Tuliona itafaa kukifasiri kwa Kiswahili kwa ajili ya wasomaji wa Afrika ya Mashariki ambao wengi wao ni wenyewe kumpenda Nabii Isa, amani ya Mungu iwe kwake, na kumheshimu kama mpendwa wa Mwenyezi Mungu.

Namshukuru Bwana Athmani Mwinyi Gakuria, mwenyekiti wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya wa Nairobi, aliyechukua jukumu la kukifasiri kwa Kiswahili chepesi na chenye kueleweka vizuri. Pia zamani alipata kutafsiri baadhi ya vitabu toka Kiingereza. Mwenyezi Mungu Amwongezee elimu, afya na umri mrefu na kuzibariki kazi zake zote njema anazozifanya kwa kuwasaidia wananchi kuuelewa ukweli.

Mimi nimepiga taipu mswada wote; hivyo nimesikia utamu wa tafsiri hii kabla ya wasomaji wengine. Maneno ya Sayyidna Ahmad, amani ya Mungu iwe kwake, nimeyafasiri kutoka Kiurdu, kwani Kiurdu na Kiswahili vinafuatana vizuri. Ni kweli ya kuwa nuru hutoka mbinguni na kuvimulika vitu vyote ardhini. Kuna vipindi maalumu vyatia giza na vingine vyatia mwangaza.

Karne ya 14 ya Kiislamu imekuwa ya baraka nyingi kwa vile ndani yake alidihihiri Masihi wa Akher zamani ambaye ndiye IMAM na KIONGOZI wa nyakati hizi. Zimeonekana ishara nyingi za kuhakikisha ukweli wa madai yake. Huu ni mwaka wa mwisho wa karne hii na baada ya mwaka huu kupita tutaingia karne ya 15 ambayo ndiyo ya heri zaidi, kwa sababu ushindi wa Dini ya Islamu utapatikana humo kwa sura iliyo waziwazi.

Nina hakika ya kuwa hiki ni kipindi cha giza kuondoka na nuru kuenea. Kweli haihitaji upanga, bali huuingia polepole akilini na kupenya moyoni. Upanga kazi yake ni kukata na kuleta kifo.

Uislamu shabaha yake ni kuunganisha watu kwa kuwaletea uzima wa kiroho na wa kiakili na wa kimwili. Huu ndiyo Uislamu unaofundishwa na wafuasi wa Masihi Aliyahidiwa, Hazrat Mirza Ghulam Ahmad A.S.

SHEIKH MUHAMMAD MUNAWWAR,
MBASHIRI MKUU,
JUMUIYA YA WAISLAMU WAAHMADIYYA,
S.L.P. 40554,
NAIROBI, KENYA.

Januari 4, 1980
Sul'hu 4, 1359
Safar 14, 1400

Kwa Jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwingi wa Ukarimu.

UTANGULIZI

Upigaji picha ni ufundi wenye manufaa kwa wanadamu; lakini manufaa yake yaliyo makubwa kabisa ni kule kutuonyesha picha ya Yesu ambayo kwa muda wa zaidi ya karne kumi na tisa zilizopita ilikuwa imenasika juu ya sanda yake kwa njia ya kiajabu.

Wakati sanda iliyofunikiwa mwili wa Yesu ilipopigwa picha hapo tarehe 28, mwezi wa Mei, mwaka wa 1898 ukawa ndiyo mwanzo wa kumwona Yesu alivyokuwa. Na huenda ndipo tulipoanza kumchunguza Yesu kwa mbinu za kisayansi. Katika harakati hizi tunapata msaada kutohana na uvumbuzi mwingi uliofanyika katika majira haya yote. Matokeo ni kuzuka kwa picha mpya ya Yesu.

Wahubiri waweza kutaharuki kwa kuambatanishwa ‘sayansi’ na ‘Yesu’ au waweza kukataa ‘uvumbuzi’ wowote wakiuita ‘mkondo mpya wa ukataaji Mungu’. Lakini hii isituzuie kufaidika kwa habari hii ya kipekee ambayo tumeletewa na Mungu kuwa zawadi ya kizazi hiki chetu.

Kitabu hiki kina sehemu mbili. Sehemu ya kwanza ni maelezo ya sanda na sehemu ya pili ni juu ya uvumbuzi mwingine. Halikadhalika kinaweka mbele ya wasomaji maoni ya Waislamu Waahmadiyyakumhusu Yesu, kikihakikisha kwambawanasayansi kamwe hawakutupatia picha mpya ya Yesu. Bali ni picha ileile ambayo Kur’ani Tukufu iliihifadhi tangu miaka 1400 kwa njia ya muhtasari na ambayo mwanzilishi wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya aliifafanua zaidi, miaka 85 iliyopita.

Tunakiweka kitabu hiki wakfu kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na tunamwomba Yeye ili kitosheleze haja ya watafutao ukweli. Amina.

April 15, 1978, Shakil Ahmad Munir
Ahmadiyya Muslim Mission
45, Idumagbo Avenue, S.L.P. 418,
Lagos, Nigeria

MLANGO WA KWANZA

SANDA YA YESU

Ille sanda iliyofunikiwa mwili wa Yesu, baada ya kuondolewa msalabani, ingalipo na yaweza kufanyiwa ziara mjini Turin, Italia. Mabaki haya ya kale yamewekwa wakfu na kuonyeshwa kwa mamilioni ya watu wa vizazi vingi. Hata hivyo haikuonyeshwa sana katika kipindi cha karne chache zilizopita. Imeendelea kuonyeshwa katika siku za Pasaka, ingawaje sasa huonyeshwa mara moja kila baada ya miaka 33.

Leo sanda hiyo imewavutia sana wanasyansi. Picha ya ajabu iliyogunduliwa katika sanda hiyo miaka 80 iliyopita, ndiyo iliyokuwa chanzo cha kiherehere kikubwa cha wanasyansi. Tokea hapo hamu yao ikazua kundi maalum la utafiti. Kwa kuzingatia mbinu za ufundi wa picha wanasyansi hao sasa wanaweza kurejea sehemu kubwa ya Injili kuhusu kisa cha msalaba na kuongeza mengine yasiyokuwamo ndani ya Injili. Kurasa zifuatazo zatoa maelezo yote.

Lakini kabla hatujazungumzia hii ‘hekaya ya karne’ hebu kwanza tuchunguze sanda na habari zake za nyuma kwa makini.

SANDA YENYEWE

Ni shuka ya kitani yenye urefu wa futi 14 na inchi 3 na upana wa futi 3 na inchi 7; na juu yake inajitokeza sura ya mwili wa mtu, mfano wa picha. Picha hii imefifia na kuchakaa na inaonyesha madoadoa na mawaa yenye rangi ya urujuani yanayofahamika kuwa ni alama za damu. Katika picha hii upo upande wa kifuani na upande wa mgongoni kwa mtu huyo ulionakilika katika sehemu mbili za sanda hiyo - hii ikionyesha kwamba sehemu moja ya shuka hiyo ilikuwa amelalia Yesu chali hali sehemu ile nyingine ikamfunika upande wa mbele. Picha yenyewe imevurugwa kidogo na alama za mikunjo na za kuungua moto na viraka. Alama hizi zinaonekana zaidi kuliko sura yenyewe ya mtu.

HISTORIA YA SANDA

(a) Nguo hii aluinunua Yosefu wa Arimataya (Marko 15:46). Yesu alipotoka mle pangoni alimokuwa amelazwa baada ya kutolewa msalabani aliiacha ndani pamoja na vitambaa vingine (Yohana 20:5-7) na akajivisha mavazi ya mlinzi wa bustani ili asitambulike (Yohana 20:15). Shuka hii iliyohifadhiwa ndiyo mabaki matakatifu.

(b) Habari za mabaki haya hazikuvuma sana katika karne tatu za awali. Kwa Wakristo wa mwanzoni huo ulikuwa wakati wa mateso na kujificha.

(c) Katika karne ya nne ambapo mfalme Konstantina alikubali Ukristo na hali ya Wakristo ikawa njema ndipo walianza kuionyesha shuka hii hadharani na kwa kawaida iliwavutia wengi. Alama za mawaa zilizo juu ya shuka hiyo ndizo zilizotia fora.

(d) Katika mwaka wa 438, malkia Endoxia alijipatia shuka hii na kuihamishia mji wake mkuu wa Kastantina. Kwa miaka mingi ilikaa katika kanisa la kifalme na ilikuwepo wakati wa vita vya nne vya Wakristo dhidi ya Waturuki ambapo mji huo uliposhambuliwa kwenye mwaka wa 1204. Mkuu wa majeshi ya uvamizi, Kapteni Othon De la Roche, akaipeleka sanda hiyo Ufaransa.

Huu ukawa mwisho wa kipindi muhimu cha historia ya sanda hiyo. Katika kuelezea habari za kipindi hiki tumepewaa msaada na maandiko ya Mtakatifu Braulio (AD 120); Askofu Arculph (AD 670); Mtakatifu John Damascene (karne ya 8); Askofu Mkuu William wa Tyre (AD 1171); Nicholas Mesoritas (AD 1204) na wengineo.

(e) Huko Ulaya tarehe ya sanda ilianza baada ya mwaka wa 1207. Nayu ni kama ifuatavyo:

Toka mwaka wa 1207 mpaka mwaka wa 1349 sanda hiyo ikawekwa katika kanisa la Basancon, Ufaransa.

Toka 1350 hadi 1452 ilikuwa mkononi mwa jamaa ya Champagne, huko huko Ufaransa. Waliweka ndani ya kanisa moja mjini Lirey lililojengwa hapo 1353. Hapo ilionyeshwa mara kwa mara.

Tangu 1452 hadi 1578 ilimilikiwa na jamii ya kifalme ya Savoy ambao waliweka kanisani pembezoni mwa jumba la kifalme. Hapo kanisa la Kirumi likatoa kibali chake kwamba sanda hiyo iwe ikionyeshwa hadharani.

Toka mwaka wa 1578 hadi leo: Mji wa Turin ulipokuwa makao makuu ya ufalme wa Savoy sanda ilihamishiwa kule ambako iko hadi leo. Hapo imehifadhiwa ndani ya kasha la fedha katika kanisa lililojengwa mahsus i kwa ajili yake. Kuba la kanisa hilo limenakishiwa na kupambwa kwa fahari ambayo haupo mfano wake katika Ulaya nzima.

(f) Ni wajibu kusema kwamba katika mwaka wa 1532 sanda hiyo iliponea chupu chupu. Jumba la mfalme wa Savoy lilipopamba moto, sanda hiyo ilikuwa ndani ya kasha la fedha ambalo sehemu yake moja ilianza kuyeyuka. Lakini yumkini Mwenyezi Mungu Alinua kuilinda sanda hii kwa ajili ya uvumbuzi muhimu katika zama zetu.

(g) Kwa mujibu wa sheria, sanda hiyo bado ni mali ya ukoo wa Savoy. Lakini kusema kweli imo mikononi mwa kanisa la Roma. Mlinzi wake hasa ni Askofu Mkuu wa jiji la Turin na ndiye anayepanga maonyesho yake kila baada ya miaka 33. Mambo yameendelea hivi hivi tangu miaka 400 iliyopita. Haionyeshwi mara kwa mara pengine kwa sababu ya kuchakaa kwake au kwa ajili ya utakatifu wake mkuu. Katika muda wote wa miaka 400 imepata kukunjuliwa na kuonyeshwa hadharani mara 21 tu vikiwemo vipindi vyaya maonyesho maalumu. (*Peter M. Rinaldi: "THE MAN IN THE SHROUD"; kilichotolewa na Sidwick & Jackson, London 1974.

*Reader's Digest, Aprili 1976.

*M.A. Faruqui: "THE CRUMBLING OF THE CROS", (kilichotolewa na Anjuman Ahmadiyya Isha'at Islam, Lahore, Pakistan.)

MLANGO WA PILI

MAELEZO YA UVUMBUZI WA MWANZO

Historia ya uvumbuzi huu ilianza hapo mwaka wa 1898 wakati wageni walipokuwa wakikusanyika huko Turin kuhudhuria maonyesho mengine ya sanda hiyo kwenye mwisho wa kipindi kingine cha miaka 33. Maonyesho yalianza mwezi wa Mei na wazo la kuipiga picha sanda hiyo likawekwa kwa nguvu mbele ya wakuu waliohusika. Kanisa halikuona ubaya wowote na likatoa kibali chake. Picha ya mwanzo ikapigwa na Secundo Pia mnamo tarehe 28, mwezi wa Mei mwaka wa 1898.

Bwana Secundo Pia akaisafisha picha yake jioni ile ile. Alipoiangalia picha hiyo kwenye mwangaza, Bwana huyo alishtuka sana hatu asiyaamini macho yake, badala ya kupata (negative) (picha ya kutolea nakala), ilitokea picha kamili (positive) na ilionyesha kwa uwazi sura kamili ya uso wa Yesu ambaye alikuwa hakuonekana tangu miaka 1900 iliyopita. Picha hii ya uso wa Yesu haikutofautiana na picha za Yesu zinazochorwa na kuenezwa na Kanisa, ILA TU, katika picha ya sanda Yesu anaonekana kuwa mwanadamu mwenye umri mkubwa zaidi ya miaka 33.

Hivyo maonyesho ya mwaka 1898 yakawa ya kihistoria. Dunia sasa ikawa imejipatia picha timamu ya Yesu ikionyesha uso wake ulivyokuwa wakati wa kusulubiwa kwake.

JAMBO JINGINE

Jambo lililoshangaza watu sasa lilikuwa ule upigaji picha wa Bwana Secundo Pia. Ilikuwaje hata picha ambayo kwa kawaida ingekuwa negative ilitokea kuwa picha kamili! Haukupita muda mrefu walipogundua kwamba SANDA NZIMA ĪLIKUWA PICHA YA NEGATIVE YA MWILI WA YESU. Lakini hakuna aliyedhania hivyo kabla Bwana Secundo kuipiga picha sanda hiyo.

Kwa ufupi, pale Bwana Seconde alipofyatua kamera yake akiilenga sanda, kitendo chake hiki kilifanya ile pitch ya negative ikiyonasika sandani kuwa pitcha kamili ndani ya kamera ile.

SWALI KUBWA

Ingawa hivyo uvumbuzi huu ulizua swali kubwa: "Ni nini kilicholeta pitcha ya negative ya mwili wa Yesu kwenye sanda hiyo?" Tatizo hili la pitcha ya ajabu likaamsha shauku mpya ya uchunguzi juu ya sanda ya Yesu na hapo kikaanza kipindi kipyga cha upelelezi juu yake. Mwanasayansi mmoja wa Kifaransa, Bwana Vignon, alikuwa karibu kulitatua tatizo hili. Baada ya jitihada kubwa iliyoendelea miaka kadhaa ndani ya maabara yake (chumba chake cha kufanyia uchunguzi), Bwana Vignon aliwasilisha rai ya kwamba ni mchanganyiko wa joto na mvuke wa gesi ya mwili aina ya "urea" pamoja na kiasi kikubwa cha manemane na ubani uliopakwa mwilini mwa Yesu na Nikodem (Yohane 19: 39) ambao ndio ukasababisha pitcha hii ya ajabu sandani iliyofanana na negative ya kawaida. Watu wengine pia wakatoa rai zao juu ya maajabu haya; lakini, maelezo kamili hayajapatikana, bado yenye kuhakikisha sababu hasa ya kufanyika hivyo. Na hali pitcha ya negative ipo mpaka sasa kama ilivyokuwa daima juu ya sanda ikithibitisha kwamba nguo hiyo iligusana kweli na mwili wa Yesu.

Picha hiyo ya negative aliyoitoa Bwana Seconde imehifadhiwa pia na hata hivi leo yaweza kuonekana katika jumba la mambo ya kale huko Turin, Italia.

Yafaa tuzingatie sana swala la umri wa Yesu. Je, ni kweli alikuwa na umri wa miaka 33 aliposulubiwa? Au umri wake ulikuwa zaidi ya miaka 45 kama pitcha yake inavyoonyesha baada ya kamera kufanya kazi yake? Umri wake unaelekea kuwa upi wakati Mayahudi walipomwambia: "WEWE HUJATIMIZA MIAKA HAMSINI BADO, NAWE UMEMWONA ABRAHAMU?" (Yohane 8: 57).

Hata ukweli uwe umesimama wapi, sanda ya Yesu imeleta mwamsho mpya katika uchunguzi wetu kuyahuusu maisha yake - uchunguzi katika misingi ya kisayansi.

MLANGO WA TATU

MAELEZO JUU YA UVUMBUZI WA PILI

Maonyesho mengine ya miaka 33 ya sanda hiyo yaliyofanywa mwezi wa Mei, 1931 yakauvutia umati wa wageni milioni mbili, yaani, watu 2,000,000 (soma THE SHROUD cha John Walch, New York, 1963). Wakati huo ufundi wa kupiga picha ulikuwa umestawi sana. Katika wakati wa maonyesho hayo fundi mpiga picha mwengine, Bwana Guisepe Enrie, akaruhusiwa na Kanisa kuipiga sanda hiyo picha mpya. Bwana huyu akitumia miali mikali ya taa za umeme alipiga picha kadha za karibu karibu na akazisafisha pamoja na kuzipanua. Matokeo yake si kwamba yaliunga mkono tu uvumbuzi wa Bwana Secundo hapo mwaka wa 1898, bali uliongeza uvumbuzi mpya; tena wa maana sana kama wa hapo awali. Ikgusia juu ya uvumbuzi huu wa pili, Jarida la The Reader's Digest, toleo la Aprili, 1976 ulisema:

Alama za vidonda kuzunguka kichwani zinakumbusha taji la miiba. Yaonekana kuwa ulipigiliwa msumari katika kiwiko cha mkono wa kushoto (kiwiko cha mkono wa kuume kimefunkwa na mkono wa kushoto). Kuna mchuruziko wa matone meusi juu ya viganja vya mikono; na vidonda vya mabegani vinaonyesha kwamba uzito mkubwa ulibebwa. Alama ya mkuki ubavuni yahakikisha yale aliyoyashuhudia Yohane kwa macho yake: "Lakini askari mmoja alimtoboa ubavuni kwa mkuki, na mara ikatoka damu na maji ..." (Yohane 19:34).

Picha za Bwana Guisepe Enrie zilitoboa mengi. Na huu ulikuwa uvumbuzi wa kipekee sana ikikumbukwa kwamba hayo yote yaliyofichuliwa yalikuwa yamefichama ndani ya sanda hiyo kwa muda wa miaka 2000.

Ni lazima tutaje ukweli wa jinsi picha hizo zinavyoyajibu maswali ambayo Yohane (20:27) amepata kuyauliza, ingawa si kwa uwazi zaidi. Anasimulia hivi:

Kisha (Yesu) akamwambia Tomaso, "Lete kidole chako hapa uitazame mikono yangu; lete mkono wako ukautie ubavuni mwangu "

- a. Je, wakati huo Yesu alikuwa akimwonyesha Tomaso viganja vya mikono yake? Kama ni hivyo, basi je, misumari iliyopigiliwa katika viganja vya mikono, ingeweza kuhimili uzani wa mwili wa Yesu?
- b. Ni upande upi wa Yesu uliochomwa mkuki? kuumeni au kushoto ulipo moyo?

Picha zilithibitisha wazi kwamba misumari ilipigiliwa katika viwiko vya mikono WALA SI KATIKA VIGANJA kama ilivyodhaniwa hapo kabla. Na mkuki ulipenya katikati ya ubavu wa 5 na 6 UPANDE WA KUUME wa mwili wa Yesu.

Mambo haya yanapoonekana kwa mara ya kwanza yanazidisha fani juu ya thamani ya sanda hiyo. Ndani yake sasa likawa limepatikana thibitisho la kisayansi juu ya maandiko mengi ya Biblia, pamoja na maelezo ya matamshi mengineyo. Kanisa sasa lingeweza kuwatangazia wapinzani wake kwamba sanda hii ya Turin ndiyo ilikuwa kweli sanda ya Yesu. Ushahidi ambao mpaka hapo haukulikana, na ulijulikana tu baada ya kupiga picha zilizopanuliwa sana, huo kamwe usingewenza kubuniwa na mwanadamu.

SHANGWE

Kwa jumla, wenyewe kustahi sanda hiyo walikuwa na shangwe na kutosheka na uvumbuzi, huu wa pili. Hususa Kanisa la Roma lilijivunia kuwa nacho kitu hiki kitakatifu ambacho sasa kimekuwa ushahidi mpya wa karne hii ya, 20 Juu ya kisa cha msalaba. Furaha kubwa aliyokuwa nayo Papa juu ya sanda hiyo BAADA YA UVUMBUZI WA PILI yaweza kupimwa kwa ujumbe wake ufuatao:

“Papa Pius XI hakuwa na shaka juu ya sanda hiyo iliyomvutia, naye kila mara alisisitizia umuhimu wa uvumbuzi huo. Katika risala yake aliyoupelekea ‘The First International Congress of Studies on the Holy Shroud’ (yaani Mkutano wa Kimataifa

wa Kwanza juu ya Sanda Takatifu) uliofanywa mjini Roma mwaka wa 1950, aliwataka waliohudhuria wajitahidi zaidi katika kueneza habari na heshima ya sanda hiyo mashuhuri na takatifu sana”.

Papa John XXIII, huku akiangalia kwa heshima sura ya uso iliyonasika sandani, alisikika akisema mara kwa mara, “Bila shaka hii ni kazi ya Bwana mwenyewe”.

Naye Papa Paulo wa sita akiwa katika ibada moja ya misa ndani ya kanisa la Mtakatifu Petro mwezi Juni, 1967 alitangaza: “Huenda ikawa ni ile sura iliyomo ndani ya sanda takatifu pekee ndiyo ituonyeshayo utu na utakatifu wa nafsi wa Yesu” (“THE MAN IN THE SHROUD” uk. 41).

Aliyosema Papa Pius wa kumi na mbili katika mkutano wa kwanza wa kimataifa juu ya sanda takatifu ilikuwa kweli kabisa. Kwani uvumbuzi uliofuatia baadaye wala haukubakiza tashwishi iwayo yoyote ya kwamba mabaki haya matakatifu - kama anavyoyaita - yametupa mwangaza mpya ambao wataalamu “wajitahidi zaidi” kuueneza duniani kote daima dawamu.

Ikumbukwe: Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya (iliyoanzishwa mwaka wa 1889) ambayo vituo vyake vyote vinaeneza kote duniani ujumbe wa amani nayo inazingatia sana umuhimu wa mwangaza huu uliowasilishwa na sanda hiyo. Jumuiya hii tayari imeandaa mkutano wa kimataifa mjini London mwezi wa Juni, 1978 ukiwa na lengo la kuzungumzia (miongoni mwa mambo mengine) uchunguzi wa sanda hiyo ya Turin. Kiongozi wa Waaminio, Hazrat Mirza Nasir Ahmad, Khalifatul Masih wa tatu, ambaye ndiye mkuu wa Jumuiya hii, amekubali kufungua mkutano huo wenye madhumuni makubwa zaidi ya mkutano mwingine wa kimataifa uliofanyiwa mjini Roma mnamo mwaka wa 1951.

Madhumuni ya mkutano huo wa London yataeleweka kwa uwazi zaidi tutakapofikia maelezo juu ya uvumbuzi wa tatu.

(Wakati wa kutafsiri mnamo mwaka 1979 mkutano huo mashuhuri uliotajwa hapo juu umeisha fanyika na ulifana sana. Khalifa Mtakatifu aliufungua rasmi na makala nyingi zenye maana sana zilisomwa na wataalamu waliotoka sehemu mbalimbali za ulimwengu huu na habari zake zilipata kuenea kila upande kwa njia ya radio, televisheni na magazeti kwa lugha nyingi. Chama cha Makanisa ya Uingereza kiliwaita wasimamizi wa mkutano huo kwa mjadala baina ya Waislamu na Wakristo na Mtukufu Khalifa alipokea wito wao huo siku ya tatu ya mkutano. Viongozi wa makanisa ya Kiprotestanti na ya Kikatoliki waliitwa kwenye maongezi ya kirafiki katika miji mikubwa ya bara zote. Viongozi hao bado wanafikiria namna ya kujibu mwito wetu. Mfasiri).

Ama kwa hakika sanda hii ni ya wale wote ambao wanafungamana na Yesu - Wayahudi, Wakristo na hata Waislamu, wote kwa pamoja; haidhuru awe ni nani anayehodhi au kuiweka hivi sasa.

Kabla hatujamaliza maelezo haya juu ya uvumbuzi wa pili, ni lazima tutaje ile heshima maalum ambayo Kanisa lilikipa kipande hiki cha nguo kwa kukiandalia maonyesho mahsusii hapo mwaka wa 1933 ikiwa ni chini ya miaka miwili baada ya maonyesho yake ya kawaida mnamo mwaka wa 1931. Hii ilifanyika ili kuandhimisha mwaka wa 1900 wa "wokovu" uliopatikana kutokana na Yesu. Hawakuwa na shaka kwamba hapakuwepo na kingine chenye kufungamana na sherehe hii ya kipekee kuliko kumbukumbu hii "inayoonekana" ya kisa cha msalaba.

MLANGO WA NNE

MAELEZO JUU YA UVUMBUZI WA TATU

Kwenye mwisho wa vita vikuu vya pili uchunguzi, zaidi ulifanywa kwenye zile alama za damu zilizomo sandani. Katika uchunguzi huu zile picha zilizopigwa wakati wa maonyesho ya sanda hiyo ya mwaka wa 1931 zilizingatiwa. Ndani ya picha hizi ambazo zilipigwa hali sanda hiyo ikiwa karibu sana na kamera wanasayansi walikuwa na shabaha ya kuchunguza mambo kadha kuhusu alama hizi za damu, kama vile:

- (a) Mitiririko yake, upande ilikoelekea mitiririko hiyo kulingana na nguvu za uvutano, jinsi damu ilivyonywewa na shuka hiyo, sehemu za majeraha na jinsi ilivyochezuruzika damu, n.k.
- (b) Madaktari walishughulikia zaidi umbile la ule mwili wa mtu ulionakilika juu ya sanda hiyo na wataalamu wa sanaa nao wakazingatia maajabu ya vile picha hiyo ilivyoweza kunakilika juu ya shuka. Baadaye taarifa kadha zilitolewa kama matokeo ya uchunguzi huu.

LAKINI

Taarifa iliyosisimua zaidi ni ile iliyotolewa na wanasayansi wa Kituo cha Uchunguzi cha Stuttgart, Ujerumani ya Magharibi. Wao walichunguza zaidi jinsi damu ilivyotiririka na vile ilivyonywewa na kitambaa hicho. Baada ya kuzichunguza picha za sanda kwa muda wa miaka minane, rai yao ikawa kwamba YESU ALIKUWA HAI PINDI ALIPOLAZWA KATIKA SANDA HIYO. Hakuwa amefia msalabani asilan.

Rai hii ilikuwa pigo kubwa kwa imani ya Kikristo. Wala hakuwepo aliyetarajia pigo kama hili. Lakini kwa vyovyyote pigo lenyewe halikuwa na budi kufika na athari yake ikabatilisha maoni yaliyokuweko kuihusu Sanda Takatifu.

Wanasayansi walithhubutuje kutoa rai kama hii? Waliona kitu

gani ndani ya alama hizo za damu hata wakafikia uamuzi huo? Ikazuka hasira na kutoamini! Lakini shauri lilikuwa limekwisha katwa na wataalamu hao wa Ujerumani!

MUHTASARI WA MAONI JUU YA UTAFITI HUO

Hapa tunaandika muhtasari wa maoni ya wataalamu hao ili tuweze kuelewa vile walivyoshughulikia kazi yao:

(a) Baada ya mwili, wa Yesu kushushwa chini na taji la miiba kuondolewa kichwani na mwili ukalazwa juu ya sanda, zile sehemu za kichwa zilizochomwa miiba zilianza kuvuja damu upya. Damu hiyo ilichuruzika na kuzama ndani ya sanda.

(b) Damu toka majeraha ya miiba juu ya paji la uso, kama zinavyoonyesha picha, ilitiririka kufuatia kunyanzi za paji la uso. Na wakati shuka ya sanda ilipofunikizwa mwili mzima wa Yesu, basi damu hii mpya ILINYWEWA NA NGUO HIYO na kusababisha mawaa katika sehemu ile ya sanda iliyofunikiza paji la uso. Ifahamike kwamba mara damu ikomapo kutiririka na kuanza kuganda KAMWE HAIWEZI KUNYWEWA NA NGUO bali huweza kushika tu nguo, na ikaukapo huweza kupukutika au kuacha mfano wa ukoko juu ya nguo. Lakini jinsi damu (ya Yesu) ilivyyotiririka na kunywewa au kuzama ndani ya sanda ni ishara iliyo wazi kwamba hakuwa amekata roho na moyo kamwe haukuacha kudunda.

(c) Katika hali ya kulazwa chali sakafuni, kama inavyoonekana pichani, mikono na paji la uso vingekuwa juu kupita sehemu zingine za mwili. Kama Yesu angalikuwa maiti damu mpya haingeliweza kutiririka sehemu hizi mbili, kama ilivyyotiririka kufuatana na ionekanavyo sandani.

(d) Kufuatana na alama za jeraha la mkuki upande wa kulia wa mwili, ni wazi kabisa kwamba dhoruba ya mkuki huo wa askari wa Kirumi aliyompiga Yesu akiwepo msalabani, haikuudhuru moyo wa Yesu hata chembe. Hivyo kazi ya moyo haikukomeshwa. (Kurt Berna: "JESUS NICHT AM KRUEZ

GESTORBEN"; kilichotolewa na Verlag Hans Naber, Stuttgart, 1957).

MCHORO MAARUFU WA BWANA RAMBRANDT

Sanda hiyo pia ni kielelezo kinachounga mkono ile picha mashuhuri kwa jina "Kushushwa Kutoka Msalabani" iliyochorwa na mchoraji wa Kidachi, Bwana Rambrandt (1606-1667). Hii yaonyesha jinsi mikono ya Yesu ilivyokuwa wakati wa kuondolewa msalabani.

Sanda hiyo yaonyesha tofauti kubwa baina ya michuruziko ya damu iliyopo juu ya mkono wa kulia na ile ya mkono wa kushoto. Damu ya mkono wa kulia yaonekana ilitiririka "kuelekea vidoleni". Mitiririko hii inamaanisha kwamba wakati mwili wa Yesu uliposhushwa toka msalabani, mkono wake wa kuume ulikuwa ukining'inia wima ubavuni.

Michuruziko ya damu ya mkono wa kushoto ilianzia katika jeraha la msumari kuelekea kwapani ingawa ilifuata njia mbili tofauti. Kwanza damu inaonekana ilianzia penye msumari wakati mkono ulipokuwa ukiambuliwa toka msalabani. Baada ya kuambuliwa inaonekana mkono huu ultumiwa kama "kishikio" cha uzito wa mwili wote, na bila shaka mkono wa kushoto ndicho kilichokuwa kitu cha mwisho kuambuliwa toka msalabani.

Na hivyo ndivyo ilivyo kufuatana na mchoro wa Bwana Rambrandt. Picha hii sasa imehifadhiwa katika Hifadhi ya Sanaa, mjini Washington.

Na michuruziko hiyo ya damu, ionekanayo pichani, ni ishara bayana kwamba mwili huo kamwe haukuwa maiti. Maana damu iliendelea kutoka wakati wa kushushwa. Na damu ya maiti huganda, haitembe hata chembe.

MAGAZETI

Magazeti ya nchi za Ulaya Magharibi yalizagaza sana habari hizi za kusisimua. Kadhalika maoni na makala mbalimbali yalitangazwa. Mhariri wa gazeti moja la Scandinavia akaandika:

“Kwa muda wa miaka minane iliyopita kikundi cha wanasayansi wa Kijerumani kimeifanyia uchunguzi sanda ya Yesu. Hivi majuzi magazeti yamepatiwa matokeo ya uchunguzi huo ... Wanasayansi hao wamemjulisha Papa juu ya uvumbuzi. Lakini Papa yu kimya. Uvumbuzi huo umefichua siri ya historia ya Kanisa Katoliki. Wakitumia ufundi wa upigaji picha, wanasayansi hao wamejaribu kuthibitisha kwamba kule kufufuka kulikoaminiwa na watu kwa muda wa miaka elfu mbili kuwa tukio la kimwujiza, hakika yake ni kwamba lilikuwa tukio la kawaida tu. Wamehakikisha kikamilifu ya kuwa Yesu kamwe hakufia msalabani”.

(Stockholm Tidininen; April 2, 1957; Mhariri: Christeriderlumd.)

MAANDIKO YA YOHANE

“Lakini walipomfikia Yesu waliona kwamba alikwisha kufa, na hivyo hawakumvunja miguu. Lakini askari mmoja alimtoboa ubavuni kwa mkuki, na mara ikatoka damu na maji” (Yohane 19:33, 34).

(a) Neno hili ‘waliona’ latuonyesha ya kwamba watu hao walimdhania Yesu kuwa ‘kafa’ kwa kuona tu hali aliyokuwemo, maana alikuwa ametulia huku kichwa chake kikiinama chini msalabani. Alikuwa katika hali ya kuzirai. Askari hawakuweza, wala hawangeliweza, kuchunguza mapigo ya moyo wake; kwani msalaba ulikuwa mrefu kupita vimo vyao.

Tunalinganisha kisa hiki na kunyongwa kwa kisasa, ambapo daktari huwepo na ala zake; naye hupima mwili wa

aliyenyonwa kabla ya kutangaza kwamba kafa. Hivyo kifo cha Yesu msalabani kina walakini.

(b) Tashwishi yetu inazidi tunapoambiwa kuwa "hawakumvunja miguu". Hili ni jambo zito mno na launga mkono ule uwezekano wa kupona kwake. (Kumbuka: Akida aliyekuwa pale baada ya kushuhudia mambo yalivyotukia alidhihirisha imani yake juu ya ukweli wa Yesu (Luka 23:47). Hivyo, hatuwezi kuepuka shaka ya upendeleo. Yaani, kwa sababu ya imani yake alimwachilia bila kumvunja mifupa na Yesu akanusurika).

(c) "Lakini askari mmoja alimtoboa ubavuni kwa mkuki". Sanda imehakikisha ya kuwa ubavu uliochomwa mkuki ulikuwa wa kuume. Hivyo jeraha hili, kama tulivyoona hapo juu, halingeweza kusababisha kifo; kwani moyo wa Yesu haukuguswa na mkuki.

(d) "... na mara ikatoka damu na maji". Ujuzi wetu wa kisasa unathibitisha kwamba hii ni dalili bayana ya uhai. Neno hili 'mara' lahakikisha kwamba kazi ya moyo ya kuizungusha damu haikuwa imekoma. Ni lazima bomba la moyo lilisukuma damu.

(e) Kisha, maneno - 'damu na maji' yanaongeza tumaini letu; kwani katika maana yake ya kawaida mchanganyiko wa damu na maji waweza kuonekana kama 'damu maji maji'. Yaani, damu iliyotiririka kwa urahisi au damu mpya maji maji sawa na damu ya mtu aliye hai. Rai hii inathibitishwa na sanda hiyo inayoonyesha kuvuja damu kwa majeraha yote, makubwa kwa madogo. Kutoka na kunywewa kwa damu mpya na nguo hiyo ni jambo lililo wazi na la kawaida hivi kwamba hapawezi kuwa na maoni dhidi ya haya juu yake. Na hii yabatilisha 'dhana' ya hapo awali kwamba Yohane alikuwa ameona damu ya mfu.

MAELEZO YA KUR'ANI TUKUFU JUU YA KUSULUBIWA KWA YESU NA HATIMAYE

Kurani Tukufu iliyoteremshwa kwa Kiarabu, yapata miaka 600 baada ya kusulubiwa kwa Yesu yatupa mwangaza mpya kumhusu Yesu.

(a) Kulingana na kauli ya Kur'ani Tukufu, Mwenyezi Mungu Alimwahidi Yesu ya kuwa yeze kamwe HATAUAWA namna walivyotaka Mayahudi, na ya kwamba kifo chake kitakuwa cha kawaida na cha heshima. Aya yenyeze yasema:

"Nao (Mayahudi) walifanya hila, na Mwenyezi Mungu Akafanya hila, na Mwenyezi Mungu ndiye bora wa wafanyao hila. (Kumbukeni) Mwenyezi Mungu Aliposema: "Ewe Isa (Yesu), kwa yakini Mimi Nitakufisha na Nitakuinua Kwangu, na Nitakutakasa na (masingizio ya) watu waliokufuru, na Nitawaweka wale waliokufuata juu ya wale waliokufuru mpaka siku ya Kiyama; kisha marudio yenu yatakuwa Kwangu, ndipo Nitawahukumuni katika yale mliyokuwa mkihitilafiana" (3:55, 56).

Ndiyo ahadi aliyopewa Yesu na Mwenyezi Mungu. Yaelekeea sana ya kuwa yeze alipewa ahadi hii kule Gethsemane alikoomba kwa machozi na kilio akihofia kwamba kifo cha msalaba kingemfutilia mbali yeze mwenyeze na silsila yake.

(b) Kurani Tukufu yadai kwamba ahadi hii ilitekelezwa barabara na ya kuwa Yesu HAKUUAWA juu ya msalaba. Imeandikwa:

"Na kusema kwao: Hakika tumemwua Masihi Isa, mwana wa Mariamu, Mtume wa Mungu; hali hawakumwua wala hawakumfisha msalabani, bali alifananishwa kwao (kama maiti). Na kwa hakika wale waliohitilafiana kwalo, yakini wana shaka nalo Wao hawajui hakika yake isipokuwa wanafuata dhana" (4:158).

(c) Kurani Tukufu, halikadhalika, yasema kwamba

hatimaye Yesu na mamake walihama Palestina wakakimbilia nchi nyingine. Kurani Tukufu yasema: "Na Tulumfanya mwana wa Mariamu na mama yake kuwa Ishara, na Tukawapa makimbilio mahali palipoinuka penye starehe na chemchem" (23:51)

MAONI YA AHMADIYYA KUHUSU YESU

Ni hivi punde tu ambapo sanda hiyo imefichua siri yake. Waila Sayyidna Ahmad a.s. ambaye ndiye mwanzilishi mtukufu wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya, aliyezaliwa na kuishi Bara Hindi (1835-1908) alidai zamani tangu mwaka wa 1895 ya kwamba Yesu alizirai tu msalabani¹ na akadhaniwa kafa (hali hawakumwua wala hawakumfisha msalabani. Na ye ye akasema kwamba, Yesu alipopata nafuu alihamia Kashmir - nchi katika Bara Hindi, inayokaliwa na wana wa Israeli. Kashmir ni nchi ya miinuko, yenyе milima na barafu, mabonde mazuri ya kijani kibichi na chemchem nyingi za maji. Nchi hii ndiyo inayolingana na maelezo ya aya 23:51 ya Kurani Tukufu iliyotajwa hapo juu.

Si hayo tu, bali katika mwaka wa 1899 Sayyidna Ahmad a.s. akaandika kitabu kizima kwa jina "Masih Hindustan Main" (Yesu Nchini India) kilichotolewa na 'The Ahmadiyya Foreign Missions Office, Rabwah, Pakistan' juu ya jambo hili. Katika

¹Miaka 70 baadaye, gazeti moja la London lasema: "Kuhusu kifo cha Yesu pengine ni kinyume cha imani ya Kikristo, lakini zipo dalili zinazoashiria ya kwamba hakika Yesu alizirai tu msalabani akadhaniwa kafa na baada ya muda wa kuzirai kupita akapata fahamu". (Sunday Times, London, Januari 24.

Kadhalika gazeti la GURDINA la hukohuko London, katika makala yake chini ya kichwa cha Maneno "Yesu alizirai tu", lasema: "Kwa kurudia maneno ya mwandishi wa karne ya pili (Baada ya Yesu kufa) "Iwapo tunaumizwa kwa kusema kweli, basi ni heri tuumie kuliko kuficha ukweli" (The Gurdian, London Oktoba 27, 1972).

kitabu hiki yeye akaeleza kikamilifu maisha ya Yesu baada ya kisa cha msalaba – kuponea chupu chupu msalabani, kutibiwa kwake, na kupata afueni, safari yake kuelekea mashariki kupitia mji wa (makabilila 10 kati ya yale 12 ambayo yalikuwa yametawanywa nje ya Palastina na wakaishi huko kama mapagani), na kifo chake cha kawaida katika hali ya uzee huko Srinagar, mji mkuu wa Kashmir. ('Sri' maana yake ni 'kichwa' na 'nagar' maana yake 'mji': yaani, Mji Mkuu).

Rai hii Sayyidna Ahmad a.s. hakuitoa kwa kukisia tu kama wafanyakyo wanavyuoni au wataalamu wengine katika shughuli zao. Katika kitabu chake hicho kilichotajwa hapo juu yeye anaongea kwa uthabiti wa ki-utume, akiwaita watu wote kwake akiwaambia ya kwamba "yeye ndiye nuru ya siku hizi za giza, bali yeye ndiye Masiha aliyetazamiwa kufika (Neno la Mbele, uk. 18). Na kwamba ni yeye aliyetabiriwa katika bishara ya miaka 1400 ya mtukufu Mtume Muhammad s.a.w. aliyesema:

"Kwa hakika mwana wa Mariamu atadhahiri, kama hakimu mwenye haki; ama hatimaye bila shaka atauvunjilia mbali msalaba"

Hoja zake dhidi ya kafara ya Yesu bado hazijakanushwa hadi sasa. Na kwa hizi hoja zake thabiti zenye kuathiri sana yeye amekwisha vunjilia mbali msalaba.

Kumbuka: Huu uvumbuzi unaotokana na sanda hiyo, ambao umefanyaika nusu karne baada ya madai ya Sayyidna Ahmad a.s., ni sehemu tu ya ushahidi unaomwunga mkono. Ushahidi wa aina nyinginezo umo katika sura ya pili ya kitabu hiki.

MLANGO WA TANO

UBISHI DHIDI YA SANDA NA DHIDI YA DALILI ZAKE

Kama tulivyoona, dalili zilizogunduliwa katika sanda hiyo ya Turin, ni kinyume na imani ya Kikristo. Kwa hivyo, kule kuzuka kwa upinzani mkali kuzihusu dalili zilizovumbuliwa, pamoja na sanda yenyewe, siyo jambo lililo kinyume na matarajio ya kawaida. Hapa chini tunaandika baadhi ya sababu kubwa za upinzani zilizopatikana:

- Ipo dalili gani ya kwamba nguo hii ni ya miaka 2000?
- Nguo ya zamani sana kiasi hiki ingewezaje kukaa mpaka leo?
- Pana uthibitisho gani kwamba mawaa yake si ya bandia?
- Tuweje na hakika ya kwamba rai ya wanasayansi wa kituo cha Utafiti cha Ujarumani inatumainika na ni sawa?

Wanasayansi hao - ambao sasa ndiyo wenye ari kubwa ya kuitetea sanda - waukabili ubishi huu. Wanasisitiza kwamba sanda ya Turin ni aina ya vitambaa vivilivo vikitumika nyakati za Yesu na mawaa yake si bandia asilan. Yawezekana pawe na "upungufu" fulani katika historia yake, lakini nguo hiyo yenyewe inayo ushahidi wa kindani wa kumnyamazisha awaye yote. Sanda hii yenyewe ni dalili tosha ya uhalisi wake.

(A) UMRI WA SANDA YA TURIN

Maoni ya Jarida la The Reader's Digest:

"Hivi majuzi Baraza la Papa lilikana baadhi ya mabaki yake maarufu. Sanda ya Turin, hata hivyo, ingali yaheshimiwa. Shuka hii yenyewe yathibitisha ukale wake. Ni kitambaa cha kitani kilichofumwa mtindo uliotumika huko Mashariki ya Kati wakati wa karne ya awali ya tarehe yetu". (The Reader's Digest, Aprili 1976, uk.50).

Jarida hilohilo lazikanusha sanda nyinginezo kwa kusema:

.... takribi sanda zingine takatifu sita hivi, nyingi zao zikionyesha picha za mwili wa mtu, zilitukuzwa katika miji mbali mbali ya Yuropa baada ya vita vya dini - zote bandia.". (uk. 51).

Hivi majuzi sanda hiyo ya Turin ilifanyiwa uchunguzi wa "Uvumbi wa Maua." (Pollen grain test) ili kugundua umri wake hasa. Katika shauri hili twasoma yafuatayo:

Profesa Max Prie, Mkuu wa Ma'mali (maabara) ya Kisayansi ya Polisi ya Zurich (Switzerland), aliifanya sanda ya Turin uchunguzi wa uvumbi uliomo ndani yake, na baada ya utafiti wa makini wa muda mrefu, akajenga ushahidi wa historia wa sanda hiyo pamoja na umri wake. Hususa yeze alivumbua chembe ndogo ndogo sana za uvumbi ambazo baada ya kuzitafiti zikagunduliwa kuwa vumbi za maua ya mimea iliyomea Palastine peke yake karne 20 zilizopita Hatimaye yeze hakuwa na shaka iwayo yoyote kuhusu uhalisi wa sanda hiyo ambayo pia ilikuwa na uvumbi wa maua ya mimea ya janibu za Kastantina (Constantinople) (Andreas Faber Kaiser: "JESUS DIED IN KASHMIR"; kilichotolewa na Gordon & Cremonesi, London, 1977, uk. 28).

Hivyo basi tunao ushahidi wa mfumo, nyuzi na uvumbi wa maua uliochunguzwa kisayansi kutuonyesha kwamba kwa kweli sanda hii ina umri wa miaka 2000.

(B) NGUO YA ZAMANI KIASI HIKI INGEWEZAJE KUKAA HATA SASA?

Hili si jambo gumu kamwe. Majumba ya vitu vya kale huko Misri na kwingineko yanavyo vitambaa vya nguo vya miaka 3000 hadi 5000 ambavyo vimedumu mpaka hivi leo. Atakuwaje mtu kustaaajabia sanda ya Turin yenye umri wa miaka 2000 tu, nayo ingalipo?

(C) JE, MAWAA YALIYOMO SANDANI NI RANGI ILIYOPAKWA?

Miongoni mwa upinzani wa zamani juu ya sanda hiyo ni hii dhana ya kwamba huenda fundi fulani alitiia mawaa ili kuifanya ya kuvutia. Jibu ni kwamba:

Zile nguo zilizoitwa “sanda takatifu” zote zilikuwa ufundi wa rangi, na ubandia wao uligunduliwa mara rangi ilipoanza kufujika na kupukutika. Sasa hakuna anayezishughulikia. Hazifanyiwi maonyesho yoyote, wala hazitarajiwi kufanyiwa uchunguzi wowote wa kisayansi. Lakini hii sanda ya Turin inayoonyeshwa mara kwa mara tangu karne nyingi zilizopita yatafautiana nazo. Siyo matokeo ya upakaji rangi wala haina alama yoyote ya rangi wala si bandia.

1. Dr. Viale, mkuu wa majumba ya kale mjini Turin na mtaalamu mashuhuri wa sanaa, asema:

“Katika miaka yote ya utaalamu wangu wa uchoraji picha, sijawahi kuona chochote kinacholingana na picha iliyomo katika sanda hiyo. Ukweli kwamba picha ya ajabu ya Yesu ilinakilika kwa njia ya negative katika sanda ya kale ni kitendawili cha ajabu ambacho sisi wataalamu wa sanaa kamwe hatuna ufumbuzi wake”. (“I SAW THE HOLY SHROUD”, kilichotolewa na Tampa, 1940, uk. 58).

2. Dr. Pierre Barbet aongea juu ya umbo la picha iliyomo sandani. Yeye alialikwa na Papa Pius XI mwenyewe ili kuichunguza nguo hiyo. Alisema:

“Mimi ni mtaalamu wa upasuaji; kwa hivyo naifahamu vivilvyo elimu ya mwili na viungo vyake ambayo nimeifunza kwa muda mrefu. Nimeshughulikia maiti kwa muda wa miaka 13 na nimetumia muda wangu wote nikiikagua miili ya walio hai. Wazo ya kwamba fundi mchoraji wa karne ya 14 angweza kufikiria, achilia mbali kuchora picha hizi za negetive latosha kumwudhi mtaalamu ye yeyote wa viungo vya mwili na mtaalamu ye yeyote wa upasuaji nawasihi hata msilizungumzie. Picha

hii ni thibitisho tosha kwamba hakuna aliyeigusa sanda hiyo isipokuwa yule aliyesulubiwa binafsi." (Barbet Fierre: "A DOCTOR AT CALVARY ; Dublin 1953, uk. 73).

(Kumbuka kuwa karne 14 ndiyo unaodhaniwa kuwa wakati wa uhalifu wa historia ya sanda hiyo ya Turin. Hivyo wapinzaani huuchukua kuwa huu ndiyo mwanzo wa mawaa yale yaliyomo sandani. Soma pia "The Shroud of Turin" cha W. Bulst, Milwaukee, America, mwaka 1956, uk. 71. Yeye pia apinga vikali dhana hii).

3. Dr. Arthur Barnes, ndani ya kitabu chake "The Holy Shroud of Turin" azungumzia juu ya picha na rangi yake nguo hiyo. Anasema:

"Kazi ya mwanadamu, hata kama imefanywa kwa ustadi mwingi na iwe katika hali ya udogo kiasi gani, ni sharti ionyeshe athari ya rangi. Yaweza kuwa kazi ya ufundi stadi hata isiweze kuchunguzika kwa macho pekee; lakini hali yake ya asili inadhihirika mara inapotazamwa kwa hadubini. Lakini picha iliyomo sandani kamwe haionyeshi athari ya rangi kupakwa. Ni kweli imo rangi inayotafautiana hapa na pale, lakini tafauti hii siyo jambo la kupangwa. Mwisho wa kila waa umenyewwa ndani ya kitamba hivi kwamba inakuwa haiwezekani kupatambua pale waa lilipoanzia na lilipoishia. Haya ni matokeo ya utaratibu wa kimaumbile; na kwa vyovyote vile haiwezekani kufanywa na mwanadamu (Bernes Arthur: "THE HOLY SHROUD OF TURIN"; Milwaukee, 1957, uk. 89 ff.)

4. Peter M. Rinaldi, makamo wa rais wa Baraza la Sanda Takatifu la huko Marekani, asema:

"Kisha madaktari wanataja kule kuzama kwa damu sandani ambako ni taratibu hasa ya kimaumbile Hata yale mawaa ya damu toka kichwani, nyuma na mbele yalitokea kwa njia ya kimaumbile hivi kwamba mmoja wa wataalamu wa madawa alipoyaona kwa mara yake ya kwanza, aliniambia: Hizi ni picha

hasa za damu." ("THE MAN IN THE SHROUD; uk. 53, 54).

5. Na juu ya uhakika wa jeraha asema:

"Madaktari wa Tume ya Kifaransa na ya Kitaliani juu ya uchunguzi wa Sanda Takatifu wote walistaajabia uhakika wa jeraha la kuumeni mwa mtu yule wa Sandani. Hawakuwa na shaka miyoni mwao ya kuwa jeraha na hata waa la damu lililosababishwa sandani yalikuwa ya aina ambayo hayangeweza kusababishwa na kinginecho minghairi ya mkuki hasa wa Kirumi." ("THE MAN IN THE SHROUD"; uk. 55).

UAMUZI WETU SISI WENYEWE

Tukiweka kando kwanza maoni haya ya wataalamu, hebu sasa natutumie akili yetu tuliyopewa na Mwenyezi Mungu ili nasi tutoe uamuzi wetu wenyewe.

Kwa sasa tunajua kwamba picha iliyomo katika sanda ya Turin ni picha ya aina ya negative, yaani, sehemu zake za kung'aa ni nyeusi, na zile za kuwa nyeusi zang'aa. Sasa tujiulize swalii: Palikuwa na haja gani ya mchoraji picha kuichora picha hii vile? Na wazo kama hili la picha ya negative lingemjiaje kichwani ilhali nyakati zile ufundi wa kupiga picha kwa kamera haukuwepo? Alilitoa wapi wazo hili?

Uwezekano wa pekee uliopo ni huu tu ya kwamba mtu fulani aliichora baada ya ufundi wa kupiga picha kwa kamera kugunduliwa. Na hapo itamaanika kwamba kitendo chenyewe kiliruhusiwa na Kanisa. Kwani katika karne zilizopita hakuna aliyejipatia fursa kwa wakati wowote ghairi ya wakati wa maonyesho ambapo mtu aliruhusiwa kuitazama kwa macho tu. Kwa hivyo wazo kwamba pengine mtu kaichora si kwamba halikubaliki tu bali ni wazo la kipuuzi. Je, wanethubutu kuchora picha juu ya sanda hiyo ili kuthibitisha kwamba Yesu kamwe hakufia msalabani? Je, wanethubutu kweli kuing'oa misingi ya dini yao wao wenyewe kwa mikono yao?

Ukweli ni kwamba mtu hawezi kuchora ama kutengeneza picha namna ya negative kwa mkono. Na endapo mtu angejaribu, basi bila shaka hangefaulu kutoa picha safi wakati negative inapopinduliwa na kutolewa picha ya kawaida. Na hapo Dr. Barnes karibu awatie kilingeni anaposema:

“Lakini hakuna mwanadamu hata hivi leo awezaye kuchora hivi japo kama awe mtaalamu wa hali ya juu wa urekebeshaji picha Kuhifadhi kitu kigumu kama vile sura ya uso na papo hapo kuifanya picha ya negative ni kitu kilichokiuka uwezo wa mwanadamu.” (THE HOLY SHROUD OF TURIN”, uk. 89 ff.).

Hivyo twaona ya kwamba ni jambo rahisi kuzua upinzani, lakini kuutetea kwa dalili bayana ni jambo gumu mno. Kama tunao uaminifu na ucha-Mungu katika nyoyo zetu tungekubali kama alivyokubali papa John XXIII, ya kwamba:

“Bila shaka hii ni kazi ya Bwana mwenyewe.”

Na ilikuwa Mungu mwenyewe Ambaye kwa hekima yake alihifadhi picha hiyo ya negative sandani ili kwamba nyakati za Masihi Aliyahidiwa picha hiyo ije iwe thibitisho bayana la uhalisi wa sanda yenyewe. Na ili ile damu iliyomo shukani - damu hasa ya Yesu - ishuhudie ya kwamba imani ya kafara ya Yesu inayoambatanishwa na kifo chake cha laana msalabani, ni imani isiyo na msingi. Ukweli huu kamwe usingewafaa watu wa kale kwani wao wasingeweza kuifafanua picha hii. Wao walikuwa hawana elimu ya ufanuzi wa siri zake zilizofichama. Wala hawangeweza kuelewa umuhimu wa kutiririka kwa damu na kuzama kwake ndani ya nguo hiyo.

D. KUTEGEMEKA KWA UTAFITI

Swali kuhusu vile tunavyoweza kuutegemea uamuzi wa Kituo cha Utafiti cha huko Ujerumani na kiasi tunachowezwa kuutumia kama msingi ni swali la maana sana. Ama kusema kweli, huu ndiyo msingi wa mazungumzo yetu yote.

Kwa bahati nzuri, kituo hicho chenyewe chatushauri tufanye

hivyo ili tuweze kutosheka. Wanatushauri kwa moyo wao wote ya kwamba tufanye juu chini tukitumia kila mbinu za uchunguzi ili tuone ikiwa twaweza kuisuta rai yao. Ni maoni yao ya kuwa "si yelete wala chochote duniani, kinachoweza kuusuta uvumbuzi wao".

Mwandishi wa kituo hicho, Bwana Kurt Berna, alichukua hatua ifaayo sana kulikabili jambo hili. Yeye alimwandikia barua Papa, kwa niaba ya kituo hicho, akimwomba amruhusu sanda hiyo ifanyiwe majaribio kamili kwa mbinu za kisayansi ili watu wayafahamu matokeo yake ni yepi.

Barua yake ambayo ilipata kutangazwa ilisema hivi:

Mtakatifu Papa Johanne. XXIII,
Vatikana, Mji wa Vatikana.
26 Februari, 1959,
Mwadhama,

Miaka miwili iliyopita Kituo cha Ujerumani cha Uchunguzi wa Sanda Takatifu inayohifadhiwa mjini Turin, kilikuwa kimewasilisha matokeo ya utafiti wake juu ya sanda hiyo kwenye Ofisi Takatifu ya Roma, na kwa wananchi wote kwa jumla. Kituo hiki chasadiki ya kwamba ulimwengu mzima kamwe hautamudu kuyapinga matokeo ya uchunguzi huu kule kuwepo kwa mchuruziko wa damu, mahali na jinsi uonekanavyo sandani, kватупатия thibitisho bayana la kisayansi na kitabibu, ya kwamba kwa mujibu wa sheria kile kinachoitwa eti kuuawa hakikutimizwa. Na kwa mujibu wa uvumbuzi huu wa sasa, mafundisho ya Kikristo, ya sasa na ya kale, siyo sahihi.

Mwadhama, hivi sasa huu ndiyo msimamo wa kisayansi kulihusu jambo hili. Ili kuusuta uvumbuzi ultiotajwa hapo mbele hatua zifuatazo zahitaji kufikiriwa:

Uchunguzi wa kisasa kwa mbinu za elimu ya kemia ili ile damu iliyobubujika kwa nguvu za mapigo ya moyo ijariubiwe kwa

madawa uchunguzi wa hadubini na majaribio mengine kama hayo sanda ichunguzwe pia chini ya nuru ya umeme (x-rays) na miali mingine ya umeme yenye nguvu nyingi Tarehe ya sanda iamuliwe kwa kutumia aina ya saa ya atomiki na pia majaribio ya "*carbon*".

"Uchunguzi huu wote utahitaji kipande kidogo tu cha sanda hiyo kama gramu 300. Hii ni sehemu ndogo sana isiyoweza kuharibu sanda hiyo wala kuitia kasoro, kwani ni kijitambaa cha upana wa sentimita 2 tu kitakachokatwa toka mapana ya sentimita 436 ya sanda hiyo."

"Hayupo Mkristo mwingine ardhini mwenye amri juu ya sanda hiyo isipokuwa wewe, uliye Papa wa Kanisa. Wala hapana njia nyingine iwezayo kuyasuta matokeo ya Kituo cha Uchunguzi cha Ujeruman, yaliyotajwa mbele, pamoja na matokeo ya uchunguzi wa watu wengine, isipokuwa kufanya haya majaribio tunayoazimia. Sielewi ni kwa nini Kanisa lisitake kuruhusu Sanda Takatifu ichunguzwe kwa njia hii. Sidhani kwamba woga ndicho chanzo cha pingamizi la Kanisa dhidi ya uchunguzi huu juu ya nguo hii ya dini. Ipo haja gani ya kuwa na woga? Kituo cha Utafiti cha Ujeruman hakina woga hata chembe; kwani kimeendesha uchunguzi huu kwa njia ya uaminifu na unyofu na kimezingatia njia zote za utafiti ziwezekanazo. Tunaweza kusema bila ya wasiwasi ya kwamba hapana yejote au chochote kiwezacho kusuta uvumbuzi huu".

"Ewe Mwadhama, twakusihi uombe dua kwa moyo wako na useme machache ili Kanisa liweze kushughulikia kazi iliyosalia. Halaiki ya wafiasi wa Kanisa pamoja na mashirika mengine yako tayari kuitikia mwito, ikiwa hii ndiyo shabaha ya Kanisa"

Salamu za unyenyekevu Mwadhama, sahihi/Kurt Berna,
Mtungaji na Mwandishi Mkatoliki,
Msimamizi wa Shughuli za Kituo cha Ujeruman. ("JESUS DIED IN KASHAMIR uk. 30-33).

Mwito huu wa huba, ambao ulitoa dhamiri ya kwamba pafanywe mpango wa kuthibitisha uvumbuzi huu muhimu wa karne hii, ulijibiwa kama ifuatavyo na “ofisi ya tawi” KUTOKA kwa Apostolische Muntiatur Deutschland.

KWA Bwana Kurt Berna
Sanduku la Posta 183
Stuttgart 1
No. 12866
BadGodsberg
13 Julai, 1959.

Iliyotangazwa katika toleo la Julai 2 la gazeti la Vatikana liitwalo “L’Osservatore Romano” chini ya kichwa cha maneno “Wokovu Halisi Utokanao na Damu ya Yesu”. Katika hii taarifa yake Papa aliwaambia makasisi Wakatoliki, walioikubali na kuizagaza habari hii, ya kwamba wokovu halisi wa wanadamu wote ulitekelezwa kwa damu ya Yesu, NA YA KWAMBA KUFA HAIKUWA LAZIMA.”

Kule kuwepo haja ya kuifafanua upya imani wakati huu lilikuwa thibitisho wazi ya kwamba yale matokeo ya uchunguzi wa Kituo cha Ujerumani yalitiwa maanani sana. Je, hili si thibitisho la kindani kwamba yale matokeo ya utafiti wa Kituo hicho yalikuwa ya kutegemewa na sawa kabisa?

MLANGO WA SITA HABARI ZINGINE KUHUSU SANDA

Kuhusu ombi lako juu ya sanda ya Turin nimeamriwa na Makao Makuu ya Serikali S. B. nikufahamishe ya kwamba Mtukufu Kadinali Maurillo Fossati, Askofu Mkuu wa Turin amekataa kuyaridhia matakwa yako.

Wako mwaminifu,
sahihi/Guido Del Mestri,
Msimamizi wa Shughuli za Makao Makuu
("THE CRUMBLING OF THE CROSS", uk.101)

Jawabu hili (alilotumiwa Bwana Berna binafsi badala ya Kituo chake) lilikuwa la kuchukiza. Kukataa huku kuliunga mkono wazo kwamba Kanisa hakika liliogopa yale ambayo yangefichuliwa kama matokeo ya uchunguzi wa aina ilioyazimiwa.

KANISA LAAINISHA IMANI YAKE

Mwaka mmoja baada ya tukio hili, Papa John XXIII alilazimika kutoa taarifa ya kufafanua "imani". Bwana A. Faber Kaiser, mtaalamu - mwandishi wa habari za dini, ameandika:

"..... Matokeo ya uchunguzi wa sanda ya Turin yamelitia Kanisa mashakani; kwa ajili hii Papa John XXIII alitoa taarifa hapo tarehe 30 Juni, 1960.

Hali ya Kanisa la Roma haikufanana na hali ya makanisa mengine; kwani Kanisa hili halingeweza kuyashuku mabaki haya yake ya thamani; wala halikuweza kuusuta uvumbuzi wa kisayansi uliotokana na sanda hiyo. Ama kwa hakika hali yao ilikuwa taabani. Ilikuwa miaka michache tu ambapo walikuwa wameisifia sana sanda hiyo na ilikuwa mwaka wa 1950 ambapo Papa Pius XII alipochagua "Tume ya Mwanzo ya Kimataifa ya Uchunguzi wa Sanda Takatifu" na akaagizia kwamba wanatume hiyo watie shime zaidi katika kuzagaza habari na heshima ya

sanda hiyo mashuhuri na mabaki hayo matakatifu sana. ("THE MAN IN THE SHROUD" uk. 41).

Hivyo wakaamua kunyamaza kimya - wakiiachia Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya kumaliza kazi iliyosalia ya kuzagaza ujuzi mpya uliopatikana kutokana na mabaki haya makuu na matakatifu. Wakayaahirisha maonyesho mengine ya miaka 33 yaliyokuwa yafanyike mwezi wa Mei 1964. Na tayari walikuwa wameukatalia mbali uchunguzi kamili wa kisayansi juu ya sanda hiyo, sawa na maazimio ya kituo cha Ujerumani. Msimamo huu uliwachukiza wapenzi wa sanda hiyo na hata wafuasi wengi wa kanisa, walioshindwa kujua kilichosababisha kimya cha kanisa na kule kuahirishwa kwa yale maonyesho yaliyo yakingojewa. Nchini Marekani likaundwa baraza lenye uwezo mkubwa likiitwa "Baraza la Sanda Takatifu" na kwalo wakaanzisha harakati za kueneza umaarufu wa Sanda hiyo kote duniani. Maneno yafuatayo yanatutobolea zaidi:

"Waaminio uhalisi wa Sanda Takatifu wana subira bali wamesononeka kwa muda mrefu. Ni miaka mingi sasa ambapo wametarajia ya kwamba Mabaki hayo - yenyeye thamani siku moja yataonyeshwa hadharani na kufanyiwa majaribio ya kibinagsi Mikutano duniani kote pamoja na wataalam wa kujitegemea wamewapelekea wakuu wanaohusika mfululizo wa nasaha: "Tunataka kumuona Yesu" (Yohane 12: 21). Lakini nasaha hizi zote ziliepwa kwa majibu ya kupigwa chenga na kimya cha wakuu hao kilichoifunikiza Sanda hiyo tangu ilipoonyeshwa mwaka wa 1933 kiliendelea mpaka hivi majuzi tu ambapo mambo yaliwachachia wakuu hao.

Ukweli ndiyo huu: Mnamo kiangazi cha mwaka wa 1969 ile subira ya waumini wa sanda hiyo ya Turin ilipata pigo kubwa wakati magazeti mashuhuri dunia nzima yalipotangaza vichwa vya maneno: Madai ya Sanda yaisuta Vatikana - Yesu Alikuwa Hai Alipozikwa - Uwongo wa Vatikana kuhusu Sanda walaaniwa n.k (THE MAN IN THE SHROUD uk 75, 76). Malalamiko ya dunia nzima yalipozidi na ule ukelele ya kwamba: "Tunataka kumwona Yesu" kupata nguvu, kanisa

likalazimika kujitutumua. Lakini utendaji wao ulikuwa mbaya kupita hata kile kimya chao.

SANDA YACHUNGUZWA NA WATAALAMU

Hawakuikunja na kufanyia Sanda hiyo maonyesho ya hadhara kama watu walivyotaka, bali walichagua halmashauri ya wataalam kuichunguza. Uchunguzi ukafanywa kwenye mwaka wa 1969 kwa njia ya siri bila ya watu ama magazeti kuwa na habari. Kisa? Eti hawakutaka maenezi. Hata hivyo habari za uchunguzi huo zilifurika na magazeti yakazitilia fora. Barua za malalamiko zilitoka ndani ya magazeti. Moja kati ya hizo ilitangazwa ndani ya gazeti mashuhuri la kikatoliki "The Tablet" kama sehemu ya makala, ikisema: Hivi majuzi magazeti makubwa nchini Uingereza na Marekani yalitangaza habari ya kwamba ile Sanda Takatifu ilifanyiwa uchunguzi kwa "siri" katika mwezi wa Juni, 1969. Magazeti hayo yamerejea karibu ile rai yote iliyoenezwa sana na Kurt Berna wa Switzerland kuihusu sanda hiyo. Bwana Berna anayo imani kwamba: "wakuu wa kanisa wanataka sanda Takatifu iangamizwe kwa maana mabaki hayo ambayo uhalisi wake umethibitika yana ushahidi usiopingika ya kwamba Yesu kamwe hakufa msalabani, na kwamba alitolewa mzima pangoni n.k." Mambo yakiwa hivyo, Bwana Berna amalizia kwa kusema, ile "ndoto" ya Ukristo ya kafara (ya Yesu) imekomeshwa milele.

Twasikitikia ukweli kwamba rai hii isiyo na msingi wala isiyohitajika imeambatanishwa na taarifa za magazeti za "Uchunguzi Rasmi" wa Sanda hiyo hususa tunasikitikia ukweli kwamba wakuu wa Turin wanaohusika hawakuwasilisha taarifa rasmi magazetini kuhusu shabaha na matokeo ya uchunguzi huo wa mwezi Juni (Gazeti la Kikatoliki, la kila wiki: The Tablet, London toleo la Juni 13, 1970).

Kumbe mwandishi huyu hakuwa na habari ya kwamba rai hii anayoiita "isiyo na msingi wala isiyohitajika" ndiyo iliyolitia Kanisa katika hali isiyovumilika na ndani kwa ndani

ikasababisha lawama ya ulimwengu juu yao na hata lawama ya mwandishi huyu. Sasa mambo yakawa kwamba Kanisa halikuiangamiza Sanda hiyo kama ilivyodhaniwa, baada ya uchunguzi wa siri wa Juni: bali walishika “mwendo mpya” kuihusu Sanda hiyo ambayo waliifahamu ni sababu ya kashfa kuliko sifa.

ASKOFU MKUU WA TURIN AHOJIWA REDIONI

Katika mwezi wa Februari 1970, ikiwa imepita miezi minane baada ya sanda hiyo kuchunguzwa na wataalamu, Askofu Mkuu wa Turin, Kadinali Pellegrina, alipoidhinisha mahojiano yake na Redio Luxembourg, katika mahojiano hayo yeye alithibitisha kuwa:

(A) “Sanda hiyo ilikuwa tayari imechunguzwa na wataalamu wa mambo ya kale, kemia, viungo vya mwili na madawa amba majina yao hayawezi kutangazwa hivi sasa ili kuwakinga kutokana na aina ya matangazo ambayo mbali na kusaidia, yankekawiza uchunguzi wao” Kadinali huyu alisema ya kwamba wataalamu hawakufikia uamuzi wowote wa mwisho kuhusu uchunguzi wao ‘kwani muda mrefu zaidi utahitajika ili kufanya uchunguzi wa ndani zaidi katika siku za usoni’, picha zilipigwa kwa kutumia vifaa bora zaidi ya vile vilivytumika karibu miaka 40 iliyopita” (THE MAN IN THE SHROUD uk 81).

Hii ilionyesha ya kwamba Kanisa lilitarajia uchunguzi “mpya” wa kindani zaidi wa Sanda hiyo bila hata kuyatangaza yale matokeo ya uchunguzi ya halmashauri ya wataalamu iliyokuwa imechaguliwa kwa ajili hii. Je, umma haukuwa na haki kujulishwa sababu au shida zinazosababisha kutofikiwa uamuzi wa mwisho wa wataalamu hao? Au wataalamu hao walifikia uamuzi nao ukawa wenye madhara sana?

(Gazeti la Times, London, lasema ya kwamba majaribio hayo ya kisayansi yalifanyika mwezi wa Juni 1969; nayo matokeo na uvumbuzi wake vikakabidhiwa Vatikana kwenye nusu

ya kwanza ya mwaka wa 1970. Ingawaje Vatikana imekataa kuyatangaza ikidai eti subira kubwa inahitajika katika mambo kama haya. (The Times, London, Mei 16, 1970).

(B) Akiendelea, Kadinali huyo aligusia zile sheria “mpya” za Kanisa kuihusu sanda hiyo. Pengine hii ndiyo iliyokuwa shabaha halisi ya mahojiano hayo. Aliizungumzia habari hii muhimu akiwa mwangalifu sana katika kila hatua.

Akianzia zile picha zilizopigwa mwaka 1969 wakati wa uchunguzi, Kadinali, alisema: Picha hizi mpya zimekuwa na MATOKEO YA MAANA. Hata hivyo, picha hizi za mwanzo mwanzo ni sharti zifuatiwe na uchunguzi wa kisayansi ambao naamini utaimarisha kuthibitishwa kwa uhalisi wa sanda hiyo” (THE MAN IN THE SHROUD uk 81).

Sehemu ya mwisho ya matamshi yake ni kidokezo cha kwanza rasmi ya kwamba Sanda hiyo haikuwa tena halisi machoni mwa Kanisa. Tena akaongeza:

“Uhalisi wa mabaki matakatifu si kitu kilichomo ndani ya maelezo ya imani ya Kanisa” (THE MAN IN THE SHROUD uk 81).

(C) Kisha akajitokeza kinaganaga kwa haya yafuatayo:

“Wala mimi sifahamu fungamano lolote lililothibitishwa baina ya SANDA HII na ile nyingine iliyokuwepo mjini Kastantina kabla ya mwaka wa 1300. (Reader’s Digest, April 1976, uk. 53).

(D) Ni la ajabu: Ile “sanda takatifu” sasa ikaja kuitwa eti “sanda hii” mara baada ya kufanyiwa uchunguzi wa siri ambao matokeo yake Vatikana ilikuwa “bado imekataa kuyatangaza”.

Kama halipo “fungamano lolote lililothibitishwa” baina ya “sanda hii” na ile iliyokuwepo kabla ya mwaka wa 1300 huko Kastantina, basi ni kwa nini inawekwa katika madhabahu matakatifu mle Kanisani ilimo mpaka leo? Ni kwa nini katika mamlaka yake yeche kama Askofu Mkuu wa Turin maamuma

(waumini) waliruhusiwa, na wangali wanaruhusiwa mpaka sasa, kuisujudia na kuiabudu “sanda hii” wakiamini kuwa ni sanda ya Bwana wao, wala hawajaelezwa eti mabaki haya bado hayajathibitishwa uhalisi wake?

Ni kwa sababu gani Papa Julius aliisalia Missa mnamo mwaka wa 1506; na ni kitu gani kilichomfanya Papa Pius VII kuisujudia akilala kifudifudi hapo mwaka wa 1814? Iliwezekanaje Papa Pius wa XI kunadi: “Tunaamini uhalisi wake; pingamizi zimekuwepo lakini hazifui dafu”? Je, nyakati zile za fahari “uhalisi” wa sanda hiyo “ulikuwemo ndani ya maelezo ya imani ya Kanisa”? Ilikuwaje hata Papa Pius XII aliita “sanda hii” kuwa “Tukufu na Mabaki Matakatifu”? Na hata akaitisha mkutano wa kimataifa kwa ajili ya sanda hiyo huko Roma? Ni kitu gani alichokiona Papa John XXIII katika “sanda hii” hata akatangaza: “Bila shaka hii ni kazi ya Bwana mwenyewe”? (“THE CRUMBLING OF THE CROSS”, uk. 87, na “THE MAN IN THE SHROUD”, uk. 41).

Mahojiano hayo kwa ujumla hayakutoa jawabu lolote, bali yalizidi kuzusha maswali mengi. Hata hivyo, Kanisa sasa likawa limevunja kimya chake cha miaka mingi. Miaka mitatu ilipita tena baada ya mahojiano haya bila ya jambo lolote la maana kutendeka. Kanisa halikutangaza tarehe ya maonyesho mengine ya Sanda yaliyotarajiwa: Hayakutangazwa matokeo ya uchunguzi wa Halmashauri ya wataalamu wa mambo ya kale, kemia, viungo vya mwili na madawa waliokuwa wamealikwa kuichunguza Sanda; wala haikuwepo fununu iwayo yoyote kuhusu tarehe ya ule uchunguzi kamili wakisayansi ulioahidiwa na Askofu Mkuu huyu.

SANDA YAONYESHWA KATIKA TELEVISHENI

Ulipofika mwaka wa 1973 shauku ya Waamerika kuihusu Sanda hiyo ikafikia kilele chake; aidha, hatua fulani zilibidi zichukuliwe baada ya yale mahojiano ya Askofu Mkuu. Kwa ghafla katika Jumapili ya Pasaka ya mwaka huo, gazeti la “New

York Times" likatangaza makala mojawapo chini ya kichwa cha maneno: SANDA YA TURIN YA KABILI UCHUNGUZI. Katika makala haya gazeti hilo liliandika:

"Ahadi imetolewa ya kuyaonyesha hadharani yale Mabaki ya ufufuo yanayolindwa sana, hii ikitangulia uchunguzi wa kisayansi."

Kuambatana na ahadi hii, Sanda ya Turin ilionyeshwa katika televisheni mnamo tarehe 24 Novemba, 1973 baada ya kucheleweshwa kwa muda wa miaka 9. Haya yalikuwa maonyesho ya dunia nzima kupitia Bahari ya Atlantiki yaliyowawezesha Waamerika wote kuiona kwa mara yao ya kwanza ile Sanda ya Yesu ya miaka 2000.

MLANGO WA SABA HATIMAYE

Ilikuwa mwaka wa 1976 tu, ambapo zilipatikana habari kuhusu ile Taarifa ya Halmashauri, iliyongojewa kwa muda mrefu.

“Ikitoa muhtasari wa matokeo ya uchunguzi uliofanywa kwa amri ya Kanisa mnamo mwaka wa 1969, taarifa moja iliyotolewa kwa magazeti mapema mwaka 1976 yasema:

“Baada ya miaka saba ya uchunguzi juu ya sanda iliyofunika mwili (wa Yesu) wanasyansi wengi wameamua ya kwamba Yesu alizikwa akiwa hai. Wataalamu hao wamethibitisha ya kwamba ile sanda Takatifu inayohifadhiwa mjini Turin ilifunika mwili uliosulubiwa na ambaa ulikuwa umeteswa sawa kabisa na Yesu, lakini wao wasema ya kwamba mtu huyu kamwe hakufia msalabani, bali alizikwa akiwa hai. Mawaa 28 ya damu yaliyomo sandani yathibitisha rai hii. Wachunguzi hao wanatuhakikishia ya kuwa maiti ikifunika sanda haiwezi kamwe kutiririka damu jinsi hii. Yesu alizikwa akiwa hai, isipokuwa kama palitokea Yesu wa pili na akateswa hivyo hivyo”. (JESUS DIED IN KASHMIR” uk. 28).

Rai kama hii ndiyo iliyotolewa na Kituo cha Uchunguzi cha Ujerumanî, miaka 20 iliyopita - “maiti ikifunika sanda haiwezi kutiririka damu jinsi hii”. Huu sasa ni ukweli uliothibitishwa na makundi mawili mbalimbali ya wachunguzi, wala si kitu cha kubishaniwa tena kadiri sayansi inavyohusika. Kitu kinachosalia ni kuthibitishwa kwa uhalisi (yaani, umri) wa nguo hiyo.

Itakumbukwa ya kwamba mbali na ule uchunguzi wa mwaka 1969 Sanda hiyo ilifanyiwa uchunguzi mwengine mwaka wa 1973 ili kukadiria umri wake hasa. Gazeti la ‘San Francisco Chronicle’ huko Marekani, lasema:

“Mwaka jana zilipokewa habari zikieleza ya kwamba uchunguzi wa sanda uliofanywa na wanasyansi wa Kiitalia katika miaka

ya 1969 na 1973 umeshindwa kusuta ukweli kwamba sanda hiyo ni ya karne ya awali" (San Francisco Chronicle, Machi 30, 1977).

SANDA KUFANYIWA MAJARIBIO YA NDANI

Majaribio haya yanayotarajiwa kufanywa katika mwezi Mei 1978 yana lengo la kuuleta pamoja utaalamu mbalimbali uhusikanao na sanda hiyo na kuthibitisha umri wa Sanda hiyo na kuifanyia aina mpya ya majaribio ambayo hajafanyiwa toka hapo. Ipo habari ya kwamba watu watakaposhiriki katika uchunguzi huu watachaguliwa kufuatia "aina ya utaalamu wao" wala si katika misingi ya kitaifa ama dini ya mtu. Mipango imo mbioni kutayarisha mradi huu mkubwa. Lile Baraza la Sanda Takatifu lililo na maskani yake mjini New York wakiwemo wanasyansi wawili kutoka Chuo cha Wanajeshi wa Anga wa Marekani, Mwingereza mmoja Kasisi aliye mtaalamu wa Agano Jipy, mwakilishi mmoja wa Vatikana na wengineo - takribu watu 30 tayari wamekwisha kukutana katika kikao cha faragha, kukagua upya mambo yalivyo na kutoa mapendekezo kuhusu mradi huo wa mwezi wa Mei, 1978.

Gazeti la 'San Francisco Chronicle' lasema:

"Walter C. McCrone ambaye ni mtaalamu wa elimu ya vitu vidogo-vidogo visivyoweza kuonekana kwa macho aliuambia mkuutano ya kwamba ile njia ya kisayansi kuamua umri wa kitu iitwayo "Carbon 14" sasa imestawishwa hivi kwamba hata kipande cha nguo hiyo cha eneo la nusu inchi chatosha kwa shughuli zetu" "Tayari vipande viwili vya ukubwa wa kutosha kwa majaribio haya ya ndani vimekwisha katwa toka sanda hiyo ..." Uchunguzi usio wa kawaida kabisa uliojadiliwa pengine ni utumiaji wa mitambo ya kompyuta ili kuzipanua sana picha za sanda hiyo katika Chuo cha Jeshi la Anga la Marekani huko Los Alamos na katika Maabara ya Vyombo vya Anga, yaani Jet Production Laboratory. (San

Francisco Chronicle, USA, Machi 30, 1977).

Hapana shaka ya kwamba endapo majoribio haya ya kuthibitisha na kupeleleza yatafanyika, yatakuwa ya thamani kubwa kwa upande wa sayansi tunapokumbuka ya kwamba ala na mbinu za kisasa zitatumwiwa.

LAKINI

Sehemu iliyio na maana zaidi ya historia ya Sanda hiyo tayari imeshatangazwa, yaani, yule aliyefunika sandani "hakufia msalabani" Tunatia maanani ukweli kwamba katika taarifa yao ya mwaka 1969 wataalamu wamejizua (na pengine hawakukosea kufanya hivyo) wasimwite "mtu huyu" Yesu. Majoribio ya Kisayansi kamwe hayawezi kutuambia eti mtu yule aliyelazwa katika Sanda hiyo alikuwa "Yesu". Bali Biblia ndiyo inayostahili kutupatia habari hii kwani picha za Sanda zadhihirisha ya kwamba "mtu huyu":

- alichapwa mijeledi (Alama za mijeledi zinaonekana pichani na zimehesabiwa).
- alibeba mzigo mzito (Alama za majeraha ya mabega zaonekana).
- alivaa taji la miba (Alama za tundu za miiba zaonekana wazi juu ya paji la uso na nyuma ya kichwa).
- alichomwa ubavuni (Alama ya jeraha katika upande wa kuume wa mwili).
- na miguu yake haikuvunjwa (Hamna alama za mivunjiko pichani).

Huu ni ushahidi tosha wa Biblia kuthibitisha ya kwamba huyu alikuwa Yesu, mwana wa Mariam, ambaye kuteswa kwake kulitabiriwa.

MLANGO WA NANE ISHARA YA YONA

Leo Sanda hiyo ni dalili ya ukweli kwamba “Yesu alizikwa akiwa hai. Hii yatukumbusha ile “Ishara ya Yona” ambayo Yesu aliahidi kuonyesha. Akizungumzia kizazi kiovu kilichotaka ishara kwake, alisema:

Watu hao wanataka kuona ishara, hawatapewa ishara nyingine, ila tu ile ishara ya nabii Yona. Jinsi Yona alivyokaa siku tatu kutwa kucha tumboni mwa nyangumi, ndivyo naye Mwana wa Mtu atakavyokaa ndani ya ardhi siku tatu kutwa kucha” (Mathayo 12:39, 40).

Yesu alitamka hayo juu ya nafsi yake mwenyewe. Lakini yeye alikaa pangoni mchana ‘mmoja’ tu, na ‘mausiku mawili’. Na hapa hakuna kufanana kamwe. Hivyo ishara ya Yona ilikuwa kitu kingine. Yona aliingia tumboni mwa nyangumi akiwa ‘hai’ akakaa humo ‘hai’ na akatoka akiwa ‘hai’. Kwahiyo ilikuwa lazima Yesu naye aingie pangoni akiwa hai, akae humo akiwa hai na kutoka tena humo akiwa hai. Yesu aliyekufa na eti akafufufu, hangeweza kamwe kuonyesha ‘Ishara ya Yona’.

Isitoshe, Yesu hangeweza kufia msalabani kwa sababu ya maombi yake mbele ya Mungu yaliyopokelewa barabara:

“Yesu alipokuwa anaishi hapa duniani, kwa kilio kikuu na machozi alisali na kumuomba Mungu ambaye alikuwa na uwezo wa kumwokoa kutoka kifo; naye alisikilizwa kwa sababu ya kumcha Mungu”. (Waebrania 5:7).

(Katikabustanihuko Getsemane Yesuhakuomba afeakafufuliwe kutoka wafu. Aliomba tu asife kifo cha laana msalabani. Katika tafsiri mpya ya Injili kwa Kiswahili iliyotolewa na United Bible Societies mnamo mwaka 1977, yameongezwa manena “kikombe cha mateso” katika Mathayo 26:39; Marko 14:35 na Luka 22:42 ambapo katika tafsiri zote za zamani “mateso” hayakupata kutajwa kokote ndani ya Injili hizi. Maneno yaliyoandikwa

ndani ya Waebrania hapo juu pia yanataja “kifo” wala siyo “mateso”; maana Yesu aliteswa kabla ya kukazwa msalabani na akateseka akiwa hapo juu ya msalaba. Hivyo tafsiri mpya inamfanya Yesu aonekane mtu ambaye hakumcha Mungu wala hakusikilizwa maombi yake; kwani alipata mateso makali, tena mengi. Hakika ni kwamba alitaka kuokolewa katika kufa juu ya msalaba na ombi lake likapokelewa kwa sababu ya kumcha Mungu. Mfasiri)

Hivyo ahadi yake ya kuonyesha Ishara ya Yona na maombi yake ya kuokolewa katika kifo yanathibitisha ukweli uliofichika muda mrefu. Twamaliza kwa kusema: Tuzitupilie mbali itikadi za kale. Ukweli sasa umebainika na damu ya Yesu, iliyogunduliwa nguoni, imetoa ushuhuda wake. Ilikuwa kweli alivyotabiri Yesu;

“Mtaujua ukweli, nao ukweli utawapeni uhuru” (Yohane 8:32).

SEHEMU YA PILI

UVUMBUZI MWINGINEO

Uvumbuzi unaoelezwa katika kurasa zifuatazo umegawanywa sehemu tatu kubwa:

- (a) Yesu kutofia msalabani na kupona kwake.
- (b) Yesu huko nchi za mashariki.
- (c) Kifo cha Yesu nchini Kashmir.

Majira ya uvumbuzi huu wote ndiyo jambo lenye maana zaidi. Sayyidna Ahmad a.s. ambaye ndiye Mwanzilishi wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya alizaliwa mwaka wa 1835; na karibu uvumbuzi huu wote ulifanyika baada ya kuzaliwa kwake. Ilikuwa kana kwamba uvumbuzi huu ulikuwa ukimsubiri azaliwe kisha nao ufanyike nyumaye ili kuyaunga mkono madai atakayoyafanya.

Sayyidna Ahmad a.s. asema:

“Mtume Mtukufu Muhammad s.a.w alibashiri akisema ya kuwa imani ya msalaba kamwe haitafifia wala maendeleo yake kukatizwa hadi pale Masihi Aliyahidiwa atapodhihiru humu duniani. Hivyo ilikuwa azma ya Mwenyezi Mungu kwamba silaha hii ing'aayo na hoja hii inayodhihirisha kweli waziwazi itolewe mkononi mwa Masihi Aliyahidiwa kwa kukomesha imani ya msalaba. Maana ndiye yeye ambaye msalaba utavunjwa nguvu yake kwa mkono wake mwenyewe.

Siri iliyokuwamo ndani ya utabiri huu ni kwamba katika wakati wa Masihi Aliyahidiwa zitapatikana sababu kwa idhini ya Mwenyezi Mungu zitakazo fafanua ukweli kuhusu tukio la msalaba. Ndipo imani hii itatimiza umri wake na kukoma. Lakini hayo hayatafanyika kwa vita na umwagaji wa damu; bali kwa njia za kimbingu zitakazoleta elimu mpya na kuwashakikishia watu ukweli ulivyo. Ndio mradi wa Hadithi inayopatikana katika Bukhari na vitabu vinginevyo. Basi, ililazimu ya kwamba

mambo haya na ushahidi, huu na ithibati hizi zisidhihirike mpaka hapo atakapofika duniani yule Masihi Aliyahidiwa kufika. Na ndivyo ilivyotokea sasa. Kuanzia hivi sasa ambapo yule aliyahidiwa ameshafika, kila jicho litafumbuliwa na wenye akili watafikiri kwani Masihi wa Mwenyezi Mungu ameshafika. Akili hazina budi sasa kupata nuru na mionyo ya watu lazima ielekee jambo hili. Kalamu zitaandika kwa nguvu zaidi na hima za wanadamu zitaimarika. Wamchao Mwenyezi Mungu sasa wataelewa na wenye akili watajaaliwa fahamu nyingi. Kwani chochote kitoacho nuru toka juu mbinguni, vilevile huangaza ardhini. Amebarikiwa yule apataye sehemu ya nuru hii na ni mwenye bahati njema aliyejaaliwa mwangaza huu. Matunda yanaiva kwa wakati wake na nuru, halikadhalika, hujitokeza wakati wake unapowadia. Hakuna awezaye kuileta nuru kabla ya wakati wake, na inapoangaza hamna awezaye kuizuia.” (Yesu nchini India, uk. 64, 65).

(A) YESU KUTOFIA MSALABANI NA KUPONA KWAKE UGUNDUZI WA MAANDIKO YA MWAKA WA AD 40 HUKO ALEXANDRIA

Hati hii yenyе maandiko yenyе kurasa zipatazo 150 iligunduliwa kwa bahati na mfanyi biashara mmoja katika mwaka wa 1873 alipokuwa katika, ziara ya kutalii Makao ya Kale ya Watawa wa Kiyunani ya wafuasi wa chama cha Waessini mjini Alexandria (ambao ni mionganoni mwa miji ya Kikristo ya awali). Baada ya kufasiriwa, maandiko hayo yakatokea kuwa taarifa ya mtu aliyeshuhudia kisa cha msalaba. Kusema kweli hii ni barua ndefu iliyoandikwa na ndugu Mwessini wa Yerusalem kwa ndugu Mwessini wa Alexandria akijibu maswali ya huyu nduguye. Ikiwa imeandikwa miaka saba tu baada ya tukio la msalaba, ni ya kale zaidi ya maandiko ya vitabu vyote vya Injili na kwa upande wa historia, huu ni ushahidi uwezao kutegemewa zaidi ya ule wa Yohane ambaye kitabu chake kiliandikwa baina ya miaka 90-120 baada ya tukio la msalaba.

Kwa mara ya kwanza barua hiyo ilifasiriwa katika Kilatini na baadaye katika lugha ya Kiingereza kwenye mwaka wa 1893. Huko Marekani kampuni moja ya vitabu ya mjini Chicago iitwayo Indo - American book Co. iliitangaza habari hii mwaka wa 1907. Kilipewa jina "Crucifixion By An Eye witness", yaani Tukio la kusulubishwa kama linavyoelezwa na shahidi aliyeliona kwa macho. Kampuni nyingine ya Kimarekani ya uenezaji wa vitabu kwa jina Austin Publishing Co. ya mjini Los Angeles, California, ikaitangaza tena habari hii katika mwaka wa 1919. Habari zaidi kuihusu barua hii zawefa kusomwa katika vitabu hivyo vilivyo tajwa.

Hapa chini tunanakili machache toka katika tafsiri hiyo ya mwaka 1907:

"Nikodemo alipoliona jeraha, likivuja maji na damu, macho yake yakajawa na tumaini jipya, na mazungumzo yake yakawa ya kutia moyo, huku akijua kimbele yatakayotukia. Akamleta Yosefu karibu na pale niliposimama, mbali kidogo na Yohane, na akatunong'oneza upesi upesi, "Marafiki wapenzi, furahini na TUFANYENI KAZI, YESU HAJAFA. Anaonekana hivi kwa sababu nguvu zake zimemuishia."

"Lakini nawasihini msimwambie Yohane tumaini letu la kuuzindua mwili wa Yesu, huenda asiweze kuficha furaha yake kuu. Na ni hatari kubwa endapo watu watalijua, kwani hapo maadui zetu wangetuua sisi sote pamoja naye".

"..... kwa kufuatia maagizo ya kistadi ya kidaktari walimkwamua taratibu, misumari ya mikononi wakaing'oa na wakamlaza chini kwa uangalifu mkubwa." Pale pale, Nikodemo akatandaza dawa ya manemane na udi pamwe na marhamu ya kuponyesha juu ya vipande virefu vya kitani alivyonunua, na ambacho matumizi yake yanafahamika baina ya wanachama wa Kiessini peke yetu. Hivi akavifunikizia mwili wa Yesu akijisingizia kwamba harakati hizi ni kwa kuuhifadhi mwili wa Yesu usioze mpaka baada ya sherehe za Sabato.

“Manukato haya ya marhamu yalikuwananguvu za kuponyesha haraka na yalitumiwa na ndugu Waessini waliozifahamu kanuni za sayansi ya utibabu kwa kuzindua watu waliokuwa katika hali ya kuzirai kulikofanana na mauti. Nao akina Yosefu na Nikodemo hali wakiinama usoni pake na machozi yao yakimdondokea, walimpulizia pumzi zao wenyewe na kupasha moto panja zake (yaani, sehemu za kichwa juu kidogo ya masikio).”

“Kisha mwili ukalazwa ndani ya pango lilichongwa katika miamba iliyo milki ya Yosefu; Baadaye wakalifukiza pango hilo kwa moshi wa manemane, udi na majani ya mimea mingine iletayo nguvu ...”

Na kumhusu malaika mwenye mavazi meupe huko pangoni, barua hiyo yatoboa:

“Mmoja wa ndugu zetu alikwenda kule pangoni akiwa amejivalia vazi jeupe la daraja la nne kuambatana na kanuni za chama. Alipitia njia ya siri tuijuayo sisi tu.

“Wale watumishi waoga wa kuhani mkuu walipomwona ndugu aliyevaa vazi jeupe akishuka polepole toka juu mlimani hali akiwemo ndani ya kungugu za alfajiri walijawa na hofu kubwa wakidhani wamejiliwa na malaika”

Ndugu yetu aliwasili kwenye pango ambalo chama kilimpa jukumu la kulilinda, alipumzika juu ja lile jiwe la mlangoni baada ya kuliondoa kufuatia amri ya chama, kuona vile maaskari wakatoroka”

Saa thelathini nyumaye:

Na ndugu yetu baada ya kusikia sauti hafifu toka pangoni, aliingia humo kupeleleza kilichotokea, Aliona kwa furaha isiyo na kifani ya kuwa ule mwili ulikuwa ukipumua na midomo yake ilichezacheza.”

Nyumaye baada ya kuwasili Yosefu na Nikodemo: “Yosefu

alimkumbatia (Yesu) akamzunguushia mikono yake - na kumweleza kisa chote na jinsi alivyonusurishwa na kifo ambacho kingesababishwa na kule kuzirai ambako kulidhaniwa na maaskari waliokuwa Calvary kwamba ni kifo chenyewe."

Yesu baadaye akahamishiwa katika kibanda humo bustanini.

Yesu alisema: "Mungu Amenizindua ili anifanye thibitisho ya yale niliyoyafundisha, nami nitawadhihirishia wanafunzi wangu ya kuwa mimi niko hai"

Kisha Yesu awaongoza wanafunzi wake hadi mlima wa Mizaituni, mahali alipopapenda sana, na akaandaa safari yake. Barua ile yaeleza:

"Na wale wanafunzi wateule waliamini ya kwamba Yesu angewaongoza mpaka Bethania. Lakini wazee wa chama walikuwa wamekutana kimya kimya upande wa pili wa mlima huo, tayari kwa safari wakisubiri Yesu akiwa mionganini mwao, kama ilivyokubaliwa hapo mbeleni."

"Na Yesu akawasihi wanafunzi wake wawe na uchangamfu na uthabiti wa imani. Akawaombea marafiki ambao punde angeachana nao na akiinua mikono yake akawabariki. Na ukungu ukaufunikiza mlima, kwani juu lilikaribia kuchwa." Lakini huko mjini ukazuka uvumi eti Yesu ameinuliwa na wingu na amekwenda mbinguni. Uvumi huu ulizushwa na wale ambao hawakuwepo Yesu alipoanza safari yake. Wanafunzi nao hawakupinga uvumi huo, kwani uliimarishe imani yao, na kuwavutia wale waliotaka kuona mwujiza ndipo wamwamini. (CRUCIFIXION BY AN EYE WITNESS kilichopigwa chapa na Indo-American Book Co. 1907 uk. 71-125).

Swali la muhimu

Biblia yakubali ya kwamba katika siku na mahali pa kusulubiwa na hata baadaye, ilikuwa ni Yosefu wa Arimathaya na Nikodemo walioshughulikia jukumu kubwa - hata la kujasiri - la kusimamia mpango wote ukiwemo mwili wa Yesu ambao

waliufanyia matayarisho yote yaliyohitajiwa ili ufaniwe maziko ya muda. Hali Mitume wa Yesu wamejiondoa, wakiwa na sababu zao nzuri.

Je, haishangazi, kwa hivyo kuona Biblia inapozungumzia kusulubiwa kwa Yesu na 'kufufuka' kwake, inarejea matamshi na maneno ya watu wa aina mbali mbali - maneno ya baadhi yao waliohudhuria (Mathayo 27.47 na Marko 15:36); ujumbe wa mke wa Pilato (Mathayo 27:19); matamshi ya akida (Marko 15:39 na Luka 23:47), maneno ya askari' (Yohane 19:24); hata maneno ya mwizi aliyetubu na yule asiyetubu (Luka 23:41,42) na baadaye maneno ya Maria Magdalena (Yohane 20:13,16). n.k.

Lakini hatuoni lolote la Yosefu ama la Nikodemus kitabu chochote cha Biblia. Kwa nini? Ni kitu gani kilichosababisha kutoandikwa kabisa matamshi toka vinywa vya watu hawa wawili walioshughulikia jukumu la muhimu zaidilenye kuhusu kisa cha msalaba? Je, waandishi wa Injili (ambao hatuwajui ni nani hao) walihofia kwamba endapo matamshi ya watu hao wawili yataingia kitabuni, basi hapo ukweli wa tukio la msalaba tulioueleza hapo juu ungefichuliwa? Wala haikufahamika kwamba siku moja yale machozi yao yaliyodondoka juu ya mwili wa mpendwa wao walipo wakiinama katika harakati za kumponya yatadhihirisha hadithi ya kweli ya mapenzi yao na ushujaa wao.

MARHAM YA YESU

Kwenye karne ya kumi na sita huko Uingereza ulipofika wakati wa kuchuma majani ya mimea iliyio ikiitwa "verbena" na "sage" ambayo ilikuwa dawa ya kuponya majeraha na vidonda ya nyakati zile, waganga walieneza habari kwamba mimea hii ina nguvu za kimwujiza za kuponyesha na "Ilikuwa mimea maalumu kabisa, kwani ilikuwa na sifa hii ya kwamba KWA MARA YA KWANZA ILIMEA HUKO CALVARY NA ILISAIDIA KUMPONYA MASIHA majeraha yake. (Mircea Eliade, 'Le Mythe du Retour Eternal' Paris, 1951).

Ni uganga wa kienyeji tu, hatuna haja ya kuuchunguza sana. Lakini twalazimika kuudadisi; kwa sababu hii yaungwa mkono na maelezo mengine yaliyotokana na njia mbalimbali. Nazo ni hizi:

(a) Twakumbuka maoni ya kitabu “Crucifixion by An Eyewitness” (yaani, Tukio la Msalaba Lilivyoelezwa na Mwenye Kuliona kwa Macho) ambayo hivi punde tumeyazungumzia ambayo yanasema:

“Palepale, Nikodemo akatandaza dawa ya manemane na udi PAMWE NA MARHAMU YA KUPONYESHA.” “manemane, udi na marhamu haya yalikuwa na nguvu ZA KUPONYA HARAKA NA MAJANI YA MIMEA MINGINE ILETAYO NGUVU” n.k.

Kule kutajwa na waganga wa Uingereza (*Peter K.Rinaldi: “THE MAN IN THE SHROUD” kilichotolewa na Sidwick & Jackson, London 1974,*Reader’s digest, April 1976, * M.A.Faruqui: “THE CRUMBLING OF THE CROSS”; Kilichotolewa na Anjuman Ahmadiyya Isha’at Islam, Lahore, Pakistan) kwa mimea iponyeshayo (ii) iliyoponyesha majeraha ya Masiha (iii) mimea ambayo ilimea huko Calvary (Mahali pakusulubiwa kwa Yesu Kristo), sio bila sababu na makusudio.

(b) Dawa hii ya kienyeji pia imetajwa katika vitabu vya utibabu kama vile: Canon of Avieccenna kilichoandikwa miaka elfu moja iliyopita na kufasiriwa kwa lugha kubwa kadha; qarabadin-e-Romi, kitabu cha maarifa ya Utibabu kilichoandikwa karibu na zama za Yesu; na vitabu kadha wa kadha vya utibabu vya zamani vimetajwa marhamu yaitwayo ‘Marham ya Yesu’ pamoja na kidokezo ya kwamba: MARHAM HAYA YALITENGEZWA NA WANAFUNZI KUYAPONYESHA MAJERAHA YA YESU.

(c) Seyyidna Ahmad a.s. aliyalishughulikia sana swala hili ameandika orodha ya zaidi ya vitabu 30 vya utibabu ambavyo viro hadi sasa vikiwa na maagizo ya matumizi ya zamani ya dawa PAMOJA NA KIDOKEZO KILICHONAKILIWA HAPO

JUU. Sayyidna Ahmad a.s. asema:

"Hata hivi leo vipo vitabu vilivyoandikwa kwa mikono ya watungaji wenyewe. Mimi binafsi ninacho nakala moja ya: Canon of Aviecenna" kilichoandikwa na mkono wakati uleule wa Aviecenna (Bu Ali Sina). Basi ni dhuluma kubwa tena ni juhud ya kuiua kweli kama tutaghafilika na ushahidi huu ung'ao. Fikirini tena na tena namna gani vitabu vinapatikana kwa Wayahudi na Wamajusi na Wakristo na Waarabu na Waajemi na Wayunani na Wajerumani na Wafaransa? Hata vinapatikana katika nchi nyinginezo za Uropa na katika maktaba ya zamani ya nchi za Asia. Haifai tuipuuze sababu hii inayoleta nuru machoni mwa watu. Kama vitabu hivi vingetungwa na Waislam au vingepatikana kwa Waislamu peke yao, huenda mtu akawaza kwa makosa tu ya kuwa Waislam walivitunga kwa kuishambulia imani ya Wakristo. Ingawaje dhana hii siyo ya kweli; kwani Waislam wamekuwa na imani sawa na Wakristo ya kwamba Yesu alikwenda mbinguni mara baada ya tukio la msalaba. Hivyo wao wasingeweza kuibuni hadithi hii iliyokinzana na imani yao wenyewe Naam, mpaka wakati wa kudhihiri Masihi Aliyeahidiwa a.s. watu hao hawakueleza fikara zao kwenye simulizi hii. Hawakuweza kupata manufaa ya kihistoria kwa jambo ambalo liliandikwa ndani ya mamia ya vitabu na kuenea kati ya watu mamilioni." (Yesu Nchini India, uk. 63, 64).

Kwahivyo, madawa haya ya kuponyesha ni thibitisho imara ya kuwa ni shughuli za kibinadamu zilizomponya Yesu wala hakufufuka kutoka wafu kwa nguvu za kimwujiza" kama waaminivyo Wakristo wengi.

KUGUNDULIWA KWA USHUHUDA WA MTAKATIFU PETRO

Tarehe 13 mwezi wa Julai, mwaka wa 1879, mzee aliye akiishi pekee alifariki mjini Yerusalem, akiacha nyuma virago vyake pangoni. Virago hivi vilipogunduliwa na alama fulani kuonekana, serikali iliwatafuta jamaa za marehemu na kuwakabidhi vitu hivyo - ambamo vilikuwemo sarafu nyingi za

kale zilizokuwa na thamani iliyokaribia Franca 200,000 pamoja na hati ya maandiko ya kale ambayo haikusomeka. Warithi hao (ambao walikuwa Wakatoliki) wakawaendea wataalamu wa maandiko ya kale. Hapo ikagunduliwa ya kuwa hati hiyo ilikuwa imeandikwa katika lugha ya Kiebrania cha kale mno. Mara wataalam hao wakavutiwa na sehemu moja ya maandiko hayo iliyokuwa ya kale zaidi iliyoishia kwa kidokezo hiki:

Mimi Petro mvuvi nimeamua kuyaandika haya kama dalili ya mapenzi juu ya jina la Yesu, KATIKA UMRI WANGU WA MIAKA TISINI, ambapo ni pasaka tatu (yaani, miaka mitatu) baada ya kifo cha kiongozi na Bwana wangu Yesu Kristo, mwana wa Mariam, kutoka Bolir, karibu na nyumba takatifu ya Bwana.”

Haya yalitangazwa na gazeti moja la Italia ya kusini liitwalo “Crierde la Sierra” katika mwaka wa 1879. Pia walidokeza ya kwamba chama cha Biblia cha London (Bible Society of London) kilipotambua uhalisi wa maandiko hayo kilitoa Lira 40,000 kuyanunua. (Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad: KISHTI-e-NUH (Safina ya Nuhu), kilichotolewa na The Ahmadiyya Foreign Missions Office, Rabwah, Pakistan, uk 102.

Ushuhuda huu wa hapo juu wahakikisha waziwazi ya kwamba Yesu alikuwa kifo cha kawaida, katika hali ya uzee mpevu. Kwani Yesu aliyeshindwa kifo kwa kufufuka toka wafu (jinsi wadaivyo Wakristo) asingaliweza kufa mara ya pili.

B. YESU HUKO NCHI YA MASHARIKI

KUGUNDULIWA KWA “UFUPISHO WA KITABU CHA MARKO”

Ukiwa unayo nakala ya Biblia isemayo kuwa:

Basi Bwana Yesu alipokwisha sema nao, akachukuliwa mbinguni, akaketi upande wa kulia wa Mungu.” (Marko

16:19), basi ufahamu, Wasahihishaji wanasesma, hiyo ni Biblia ya kale. Aya za mwisho (9-20) za kitabu cha Marko sasa si sehemu ya Biblia. Imegunduliwa ya kuwa aya hizo za mwisho ni “nyongeza” ya zama za nyuma.

Badala yake wasahihishaji wametoa “ufupisho” wa mwisho wa kitabu hicho usemao:

“Bali walimdokezea Petro na wale waliokuwa pamoja nae yote yale waliyambiwa. Na baada ya haya, Yesu mwenyewe binafsi KWA NJIA YA HAO, AKATOA TANGAZO la ujumbe mtakatifu, usio na mwisho, na wokofu wa milele, TOKA MASHARIKI HATA MAGHARIBI.” (Tafsiri ya Biblia kwa Kiingereza inayoitwa Revised Standard Version (RSV), ambayo ilitolewa mwezi wa Septemba mwaka wa 1952; na the New World Translation of the Holy Scriptures (yaani Tafsiri mpya ya Ulimwengu ya Maandiko Matakatifu iliyosahihishwa mwaka wa 1961).

Maneno “Yesu mwenyewe binafsi kwa njia ya hao, akatoa tangazo toka Mashariki hata Magharibi” yanaonyesha ya kwamba Yesu alikwenda mwenyewe nchi za Mashariki; ambapo “kwa njia ya hao” wanafunzi alipeleka ujumbe wa wokofu kwa Mayahudi waliokaa nchi za Magharibi. Tukiweka koma (,) baina ya maneno ya kiingereza “East” (Mashariki) na “West” (Magharibi), maana ya ufupisho huo wa kitabu cha Marko inakuwa wazi zaidi.

Ama kwa hakika huu ni wakati wa uvumbuzi wa masahihisho. Maandiko ya kale sana ya kitabu cha Marko sasa yamegunduliwa toka mlima wa Athosi, huko Uyunani, na kulingana kwa maneno yake ni kama ifuatayo:

NA BAADA YA HAYO, YESU MWENYEWE BINAFSI AKADHIHIRI KUTOKA MASHARIKI na hadi Magharibi, kwa njia ya hao, akatoa tangazo la ujumbe mtakatifu usiobadilika wa wokofu wa milele.” (C.R Gregory: “CANON AND THE TEXT OF NEW TESTAMENT”).

(Pengine “kwa njia ya hao” wanafunzi akapeleka onyo huko Magharibi dhidi ya kuchafuliwa kwa ujumbe wake mtakatifu kwa itikadi ngeni ya ‘kafara’ isiyo na msingi katika sheria yoyote ya Mungu).

Sisi tunasema hivi: Pana haja gani ya kukubali nusu ya ukweli baada ya kuutambua? Ikiwa ni lazima kufupisha mwisho wa Marko (mlango 16) kwa kuondoa aya ya 9 hadi 20 na kisha kupachika mwisho mpya, kwa nini isiwekwe alama hii ya koma (.) mahali ipasapo, na kuukubali ukweli wote? Lazima tukiri Yesu alikwenda nchi za Mashariki na alipopata habari ya kuharibiwa kwa mafundisho yake safi, aliwaonya wale waliohusika na uchafuzi huo wakome mara moja. Kama wao hawakujali, si kosa la Yesu!

KUGUNDULIWA KWA “ACTA THOMAETA” (MATENDO YA THOMA)

Katika siku za mwanzo za Ukristo, hiki kilikuwa miongoni mwa vitabu vilivyosomwa makanisani; Kwenye mwaka wa 495 A.D kitabu hiki kikaitwa “uzushi” kwa amri ya Papa Galasius. Polepole kitabu hicho kikaachwa na kusahauliwa. Kilipogunduliwa tena, tafsiri yake katika lugha ya sasa ikaandikwa na ikapigwa chapa katika mwaka wa 1832. Bwana Williams Wright akaandika tafsiri yake ya kwanza kwa lugha ya kiingereza na ikaenezwa na Williams Horgate wa London katika mwaka wa 1871 (kwa jina la Matendo Yasiyokubaliwa). Tafsiri nyine kadha zilitokea baada ya hapo. Hivi majuzi kundi la wanachuoni wa Kiholanzi waliandika maelezo juu yake.

Kugundulika huko kwa “Matendo ya Thomaso” kwafikiriwa kuwa ni hatua kubwa katika upande wa kujua historia ya Yesu na maisha yake.

YESU HUKO TAXILA

Kutokana na kitabu hicho cha Matendo ya Tomaso, tumeweza kujua jambo moja muhimu, nalo ni kwamba Bikira Mariam na Yesu na Tomaso walikuwa pamoja huko Taxila, ambao hivi sasa ni mji mashuhuri wa kihistoria huko Pakistan. Kitabu hicho chaonyesha ya kuwa Tomaso (pia akiitwa Judasi Tomaso) pamoja na Yesu, walihudhuria harusi ya binti mfalme Gondaphares wa India, aliyetawala eneo hilo toka 20 A.D. hadi 50 A.D akifanya Taxila kuwa mji mkuu wa serikali yake. Kifungu kimoja cha matendo ya Tomaso chasomeka hivi:

"Na mfalme akawashauri wasaidizi wa bwana Harusi waende rje ya chumba cha harusi Bwana Harusi akainua pazia ili amlete bi harusi, na akaona kama alivyodhania - Tomaso amesimama huko akiongea na bibi harusi. Bwana harusi akamwuliza: "Mbona ungalipo hapa; si nimekuona ukitoka nje?" Naye akajibu: "Mimi siye Tomaso bali ni nduguye." Na bwana wetu akakaa juu ya kitanda na kuwaacha vijana wale wakae kitini (A.F.J. Klijn: THE ACTS OF THOMAS"; Leiden, kilichotolewa na B.J. Brill, 1962, uk. 70 kifungu cha 11. Vile vile tazameni "ACTAE THOMAE" katika Biblioteca Christiana Ante Nicene, Jalada la 20, chini ya kichwa cha maneno: Syriaic Documents of the first three centuries).

(Si ajabu huyo Tomaso kuitwa 'Pacha wa Yesu' (Yohana 20:24). Walikuwa na sura za kufanana hivi kwamba watu hawakuweza kuwatofautisha kwa urahisi).

Swala muhimu lazuka hapa: Palikuwepo na sababu gani nyingineyo iliyomfanya mwandishi wa kitabu hiki kuwabaini Yesu na Tomaso wakiwa India na Pakistan, kama haikuwa kweli tupu? Twaweza kuelewa wazi kile kilichosababisha kutupwa kwa kitabu hiki nje ya Kanisa kwa amri ya Papa Galasius.

KABURI LA MTAKATIFU THOMASO

Mapapa wa siku hizi wamekubali, kwa kiasi, ukweli wenyewe (Papa Paul V; Papa Leo XIII; Papa Pius XII na wengineo). Wamethibitisha ule ukweki wa kihistoria ya kuwa Tomaso aliishi na kuhubiri Bara Hindi na akafia huko huko. Papa Pius XII (ambaye ule mukutano wa kwanza wa Kimataifa kuihusu Sanda Takatifu ulifanywa wakati wa uongozi wake katika mwaka wa 1950) alipota amri kwenye mwaka wa 1956, alitangaza:

“Nchi ile mashuhuri iitwayo India: Historia yatwambia ya kuwa hiyo ndiyo iliyokuwa nchi ya mahubiri ya Mtakatifu Mtume Tomaso, akaijaza kwa dini ya Kikristo na akaitukuza kwa miujiza yake na kifo cha fahari cha shahidi Akazikwa kule kule katika pango naye ametunukiwa heshima kubwa. Mahali Mtume yule alipoweka msingi wa kanisa dogo ndipo kanisa la kwanza lilipojengwa na Wakristu Kanisa hilo la Mtakatifu Tomaso, tayari limeshawekwa wakfu Tumeamua kulipamba Kanisa hilo kuu la dayosisi kuu ya Madras na Mylapore huko India na kulitunukia cheo cha Basilica ndogo likiwa na mamlaka kamili juu ya ibada zote za kidini zinazokihu cheo hicho”

Imeamriwa toka Roma mahala pa Mtakatifu Petro chini ya pete ya Mv уни, siku ya kumi na sita ya mwezi Machi katika mwaka elfu moja na hamsini na sita, mwaka wa kumi na nane wa utawala wetu wa Kipapa. Kwa ruhusa maalum ya Yule Mtakatifu zaidi (Kwa ajili ya hukumu nzima, someni: HISTORICAL NOTES ON ST. THOMAS" kilichotungwa na Mgr. Alberto Persira de Andrede, chapatikana kwa San Thome, Madras; India, uk 48, 49).

Hivyo Ulimwengu “sasa” umekubali ya kwamba yule ndugu pacha wa Yesu amezikwa huko Bara Hindi. Haitachukua muda mrefu ambapo ulimwengu utakubali vivyo hivyo kumhusu Yesu ambaye kaburi lake liko huko Kashmir katika “nchi ile mashuhuri iitwayo India”.

KUGUNDULIWA KWA MAANDIKO HUKO NAG HAMMADI KATIKA KINGO ZA SEHEMU ZA JUU ZA MTO NILE

Ulikuwa mwaka wa 1945 ambapo:

“Wenyeji waligundua hivyo walipokuwa katika harakati zao za kutafuta katika mapango aina ya mbolea ya kinyesi cha popo na ndege wengine iliyokusanyika huko kwa karne nyingi. Katika pango moja lililokuwa katikati ya urefu wa genge moja na ambalo njia ya pekee ya kulilifikia ilibidi kumteremsha mtu kwa kamba kutoka kilele cha genge hilo, walipata gudulia kubwa, ndani yake vilikuwemo vitabu kumi na vitatu vya jalada ya ngozi vilivyokuwa katika hali ya kuhifadhiha Wakulima hao wasiojua kusoma wakatumia vitabu viwili kama kuni za kupikia chai na vile vingine wakaviuza kwa bei (waliodhania kuwa) kubwa mno ya pauni tatu ya Kimisri (Rev. Fr. Dr. Charles Potter: “FROM THE DEAD SEA SCROLLS AND NAG - HAMMAD DISCOVERIES - THE LOST YEARS OF JESUS REVEALED” kilichotolewa na Fawoett Gold Medal Book, Fawoett, Greenwich, Conn. U.S.A., 1962 uk. 148).

Hazinahiyoiilyokwanajumlayavitabu49vitano vilihamishiwa nchi ya Uswisi kinyume cha haki - sasa ni mali ya coptic, mjini Cairo. Kazi ya kuvifasiri vitabu hivyo sasa inaendelea, lakini mingoni mwa vile ambavyo tayari vimefasiriwa; ni kimoja “Injili ya Filipo” ambayo tangu mwanzo iliandikwa kwa lugha ya Aramaic ambayo ndiyo ilikuwa lugha ya Yesu. Injili hii inayo maneno mengi ya Yesu aliyoyatamka baada ya kusulubiwa kwake, nayo haiungi mkono itikadi ya “kufufuka” kwa Yesu katika wafu. Kitabu hiki chaonyesha ya kwamba mara baada ya Yesu kumchagua James kuwa mwakilishi wake, alisafiri kuelekea upande wa Mashariki pamoja na mamake na Mariamu Magdalena. Wakati ilipotangazwa tafsiri ya kitabu hicho kwa lugha ya Kiingereza, gazeti la Times la huko London, likitoa maoni yake juu ya Injili hiyo lilisema:

“Lakini hangekuwepo muumini halisi ambaye angelikubali

makosa ya Filipo katika mafundisho yake ya kwamba Mariam Magdalena alikuwa mke wa Yesu. NI WAZI KABISA KWAMBA MMOJA WA WALE WANAWAKE WAWILI WALIOANDAMANA NA YESU ALIPOHAMIA NCHI ZA MASHARIKI BAADA YA KISA CHA MSALABA, alikuwa Mariam mamake Yesu, hali yule mwingine ni lazima alikuwa Mariam Magdalena, mkewe Yesu” (The Times of London, Machi 8, 1963).

“Mariam Magdalene awe alikuwa mke wa Yesu au la, yeye kweli alikuwa na sikitiko la mapenzi na huba maalum kumhusu Yesu (Yohane 20:11-16), wala haliwi jambo la kushangaza kwa hivyo, endapo hata yeye alielekea Mashariki aliko kwenda Yesu.

Sasa yapo makaburi mawili pembezoni mwa nchi ya Kashmir, moja katika Kashghar (Uchina ya kusini) na lile lingine lipo katika sehemu ya Punjab, mahali paitwapo “Mari”, ambao ni mji wa milimani nchini Pakistan, zikiwepo hadithi ya kuwa Mariam alizikwa pale. Na makaburi yote hayo mawili yanaaheshimiwa sana na wenyeji wa sehemu zile. La ajabu ni kwamba kaburi lile la “Mari” lipo maili 40 tu toka mji wa Taxila, mahali ambapo Yesu na Toamso walihudhuria harusi, kama tulivyoeleza mbeleni.

Je huu ulikuwa mlingano wa bahati nasibu ya kuwa Injili iliyoandikwa kwa lugha ya Yesu iliyogunduliwa huko Misri inaongea juu ya akina Mariam wawili waliosafiri kuelekea upande wa Mashariki, na ya kwamba yako makaburi mawili huko Mashariki ya akina Mariam wawili waliozikwa kule?

Au pamoja na lile kaburi la Mtakatifu Tomaso nchini India, ni dhihirisho ya kwamba uwanja wa mahubiri ulikuwa umehamishwa toka Palastina hadi Kashmir? (Kashmir pia ni sehemu ya India na inatawaliwa na serikali ileile moja ya India).

KUGUNDULIWA KWA HATI ZA MAANDIKO KARIBU NA BAHARI YA CHUMVI (DEAD SEA)

Mwaka wa 1947 ulikuwa mwaka wa shani, kwani ndiyo ulikuwa mwanzo wa ugunduzi wa hati za maandiko ya kale kwenye sehemu za Bahari ya Chumvi. Mahali pa ugunduzi wa mwanzo lilikuwa Bonde la Qumrani, lililo mashariki ya mji wa Yerusalem. Hati hizo za maandiko ya kale ziligunduliwa mapangoni zikiwa zimeviringishwa ndani ya magudulia, baadhi ya magudulia hayo yalivunjwa na mabedui, walipoya fungua kwa hamaki, wakitumainia kupata sarafu za kale kutoka humo. Magudulia kadha yalikuwa mazima hali yale mengine yalivunjika humo mapangoni.

Ukunjuaji wa hati hizo za kale zilizoviringika haukuwa rahisi. Baadhi yao ilibidi zikatwe vipande vipande. Njia iliyotumiwa ilikuwa kuingiza kibao cha mviringo katikati ya kila bunda la kurasa za hati hizo zilizoviringika, kisha kuzipulizia aina fulani ya gundi litumikalo katika uundaji wa ndege, halafu kuzikausha mpaka ziwe ngumu (kavu); kulikoziwezesha zipasuliwe vipande vipande (kama vile kupasua mbao toka gogola mviringo) kwa kutumia msumeno mwembamba sana wa mviringo. Hapo vile vipande vilivyopatikana viliunganishwa, kurasa baada ya kurasa, na vikapigwa picha” (Gazeti la ‘New York Times’, Februari 25, 1956).

Palikuwa na haja gani?

Utangulizi wa Biblia yenye we watoa majibu. Utangulizi huo wasema:

“Ilipofika katikati ya karne ya kumi na tisa, maendeleo ya kuichunguza Biblia na ugunduzi wa maandiko ya kale yaliyokuwa msingi wa ile tafsiri ya Mfalme James vilidhihirisha wazi ya kwamba makosa haya ni MENGI MNO TENA MAKUBWA MNO hivi kwamba yanahitaji masahihisho.”

(The Bible, RSV 1952 edition, Preface p. vi; yaani Utangulizi,

uk. vi mwanzoni mwa Biblia iliyofasiriwa katika Kiingereza na kupewa jina la Revised Standard Version: Tafsiri Yenye Kusahihishwa Upya ili kutumiwa na Makanisa Yote).

Matokeo yake yakawa kwamba Biblia ikasahihishwa kwenye miaka ya 1881-1885; na ikasahihishwa tena mwaka wa 1901.

Lakini ikatokea kwamba masahihisho yote haya kumbe hayakuwa ya shinani. Huu ulikuwa ni mwanzo tu, kwa sababu;

“Yale maandiko ya kale kupita yote HAYAKUGUNDULIWA MPAKA ULIPOFIKA mwaka wa 1931.” (The Bible, RSV, utangulizi, uk. ix)

Kwa hivi Agano Jipyä lililazimika kusahihishwa TENA katika mwaka wa 1946.

KUGUNDULIWA KWA HATI YA MAANDIKO

Kabla hawajamaliza masahihisho tuliyoyataja hapo juu, mara kukagunduliwa maandiko ya kale karibu na bahari ya Chumvi, huu ulikuwa sawa na ugunduzi wa hazina kuu. Hapa lilikuwa lundo kubwa la hati za maandiko ya kale zilizozikwa wakati wa machafuko ya mwaka wa 70 A.D. Hivyo basi, maandiko hayo yalisifiwa na kupokelewa kwa shangwe.

Kama asemavyo Dr. Charles Potter:

“Waumini wa zaidi ya dhehebu moja walikuwa na nderemo mara yalipogunduliwa maandiko hayo, WAKIFIKIRIA MUNGU MWENYEWE NDIYE ALIYEZIHIFADHI nakala hizo za vitabu vya Biblia kama vile Isaya yakiwa ni maandiko ya miaka elfu moja zamani kuliko maandiko mengine yoyote, yaliyokijulikana.” (Rev. Fr. Dr. Charles Potter: “FROM THE DEAD SEA SCROLLS AND NAG - HAMMAD DISCOVERIES - THE LOST YEARS OF JESUS REVEALED” kilichotolewa na Fawoett Gold Medal Book, Fawoett, Greenwich, Conn. U.S.A., 1962 uk. 14).

Wakaanza masahihisho mengine kwa juhudi kubwa na wakatangaza Agano la Kale. Tafsiri hiyo ikatangazwa mnamo mwaka 1952 na kufanywa mali ya wasahihishaji wake. Yaani hakuna mtu aliruhusiwa kuinakili bila ya idhini yao.

Agano Jipywa lilikuwa bado kurudiwa na kufanyiwa masahihisho.

Lakini kadri mapango mengine yalivyogunduliwa na maandiko mengine kufasiriwa, ndivyo shuku ilivyozidi kuongezeka ya kwamba masahihisho zaidi ya Agano Jipywa huenda yakaidhuru Dini iliyokuwepo ya Ukristo. Tunaposoma maoni ya Dr. Potter, twaweza kukisia kiasi cha masahihisho ambayo ingekuwa ya lazima kuyafanya kama Maandiko yaliyogunduliwa pembezoni mwa Bahari ya Chumvi yangetambuliwa kikamilifu. Yeye asema:

Kwa mujibu wa Maandiko yale yaliyogunduliwa huko Qumran hapana hata kitabu kimoja cha Agano la Kale kisichohitaji masahihisho na matengenezo ya hali ya kusomeka kwake wala hakipo kitabu hata kimoja cha Agano Jipywa (Habari Njema kwa Watu Wote) ambacho hakitalazimika kupinduliwa maana ya aya zake kuu zilizo nguzo za imani. Ilhali ni Wakristo wachache tu wanaofahamu (kwani ni wataalamu haba wanaokiri) ni itikadi ngapi muhimu zitakazobadilishwa kabisa, ni ngapi nyingine ambazo mwishoni zitalazimika kutupwa nje pindi hati hizo zitakapotambuliwa rasmi na kuthibitishwa kuhusiana na Agano Jipywa." (Rev. Fr. Dr. Charles Potter: "FROM THE DEAD SEA SCROLLS AND NAG - HAMMAD DISCOVERIES - THE LOST YEARS OF JESUS REVEALED" kilichotolewa na Fawoett Gold Medal Book, Fawoett, Greenwich, Conn. U.S.A., 1962 uk. 15, 16).

Miongoni mwa wataalamu mashuhuri wa maandiko hayo ya kale ni Dupont Sommers wa Chuo Kikuu cha Paris. Juhudi zake zinastahili kutambuliwa na kuthaminiwa na wote katika uwanja huu. Yeye asema:

"Matatizo yote yahusikanayo na Ukristo wa kale TANGU LEO ya ukabili MWANGAZA MPYA unaotulazimisha tuyafikirie YOTE kwa mara nyingine tena." (Dupont Sommers: "DEAD SEA SCROLLS - A PRELIMINARY SURVEY" kilichotolewa na Basil Blackwell, Oxford 1952, uk. 100).

Mlinganisho na Sanda

Twalinganisha habari hii ya Hati za Bahari ya Chumvi na ile habari ya Sanda ya Turin; tukikumbuka jinsi ugunduzi wa mwanzomwanzo kuto kana na Sanda Takatifu ulivyoshangiliwa. Lakini mara ugunduzi uliposogea kuelekea kileleni na kuanza kukosoa misingi ya Imani ya Kikristo ijulikanayo siku hizi, wao wakazua hoja kushuku uhalisi wa nguo hiyo waliyoisujudia na kuitabaruki tangu zama za kale.

Hapa pia maoni ya mwanzo ya wanachuoni wa Kikristo yalikuwa kwamba: "Mungu mwenyewe ndiye aliyezihifadhi nakala hizo za vitabu vya Biblia." Lakini nyumaye wakaanza kuzusha shuku kuhusu tarehe ya maandiko haya.

Hata hivyo shuku zao hazikuwa na msingi nao wakashindwa vibaya katika vita hivi vya kwanza, kama waviitavyo; kwa sababu ya ushahidi wa mbinu za kitaalamu zijulikanazo kama majoribio ya "PALEOGRAPHY, ARCHEOLOGY, NUMISMATICS (yaani, kulinganisha maandishi ya hati hizi na maandishi ya kale na kujaribu kukisia umri wake na uhalisi wake)" na majoribio mengineyo yaliyofanywa na wataalamu wa Idara ya Nguvu za Nuklia ya Chuo Kikuu cha Chicago (Marekani). (Powel Davies, wa All Souls Church Washington: "THE MEANING OF THE DEAD SEA SCROLLS", Mentor Book 1956, Library of Congress, Cat. Card No. 56 - 9787, uk. 26-41).

Vita vya Pili vya Hati hizo za Bahari ya Chumvi sasa vimo "mbaroni". Vita hivi vyahusu athari ya maandiko hayo juu ya

“chanzo cha Ukristo”, au tukirahisisha zaidi twaweza kusema: hivi ni vita kati ya “dini” na “historia”, kama asemavyo Powell Davies, mwandishi wa kitabu kiitwacho “The Meaning of the Dead Sea Scrolls”.

“Kwahivyo. “Vita vya Pili vya Hati za Maandiko” si vita ambavyo makasisi waweza kuvishinda. Huenda vita hivi vikawa vyenye kukata shauri la mwisho kabisa kuhusu shauri la mashindano baina ya dini na historia kwa jumla. Sifa mojawapo iyafanyayo maandiko hayo yasipingike ni kule kudhihiri kwao hivi kwamba yanaweza kuguswa na kushikwa. Kwani yapo” (Powel Davies, wa All Souls Church Washington: “THE MEANING OF THE DEAD SEA SCROLLS”, Mentor Book 1956, Library of Congress, Cat. Card No. 56- 9787, uk. 95).

Lakini “huenda ikachukua muda kadhaa watu wote kujulishwa kwa ujumla rai zilizomo”. “Bila shaka wataalamu wanaohusika na kufasiriwa kwa maandiko hayo ya kale wanachelea kuvunjika kwa imani ya mamilioni ya watu”. Ni lazima shauri likatwe kwanza mtu wa kawaida “aambiwe namna gani juu ya maandiko yaliyopatikana mapangoni, na aambiwe lini na kupewa elimu kiasi gani, au ufuatwe utaratibu gani kwa kumjulisha habari zake zote”.

HATI HIZI ZA MAANDIKO YA KALE ZATHIBITISHA MAMBO MATATU:

- (a) Kwamba Yesu alihusiana sana na chama cha Kiessini;
- (b) Kwamba itikadi za Kikristo za siku hizi hawakuzijua Yesu na wanafunzi wake hata mmoja, bali zilifahamika kwa makabila ya wapagani walio wakiishi Palastina na pembezoni mwake;
- (c) Kwamba Yesu aliondoka Palastina na kuhamia nchi nyininge.

ZABURI ZA SHUKURANI

Miongono mwa vitabu vilivyogunduliwa karibu na Bahari ya Chumvi kipo kimoja kiitwacho "Zaburi ya Shukrani" ya mwalimu mkuu wa haki na ucha Mungu. Baadhi ya aya zake zasema:

"Ewe Bwana Wewe kwa kweli utamtakuza mwana wa Mjakazi wako (Mjakazi wa Mungu maana yake ni Mariamu Luka 1:46-48). Wewe UMEYAOKOA MAISHA YA MNYONGE HUYU WALIYETAKA KUMWAGA DAMU YAKE, wakitaka kujivuna eti wao ndio wanaokutumikia Wewe Lakini Ewe Bwana wangu! Wewe Ukamnusuru mnyonge huyu asiye na uwezo dhidi ya mikono ya wenyе nguvu. Na Wewe ndiwe Uliyenipanguvunisikufurukwakutupilia mbali utumishi Wako, nikiogopa NJAMA ZAONA HILA ZAO ZA KUWACHOCHEA WARUMI" (Zaburi, namba 4) "NIMEFUKUZWA TOKA KWETU kama ndege toka kiota chake. Marafiki zangu na ndugu zangu wameniacha. Kwao mimi si zaidi ya chombo kilichovunjika. Lakini Ewe Bwana, hakika utavunjilia mbali hila za mashetani" (Zaburi namba 8).

Nakusifu ewe Bwana! kwa vile HUKUNIACHA PEKE YANGU KWENYE SAFARI YANGU KATIKA NCHI NGENI Wewe kwa hakika Utakuwa mwamba wangu katika hali yangu ya dhiki. Wewe ULIYENILETA HADI NCHI YA MBALI, bila shaka Utanikinga dhidi ya wanaadamu (wasinidhuru na kuniangamiza)" (Zaburi namba 10) .

Je, hii haionyeshi ya kwamba wale waliofanya njama na wakachochaea Warumi wakadhamiria kumwaga damu ya Mwana wa Bikira Mariam na kumwua, mwishowe walishindwa; kwani Mungu alimnusurisha na kumpeleka nchi ngeni ya mbali ili kumlinda na madhara ya watu?

Na je, Yesu mwenyewe hakuwadokezea wanafunzi wake, alipokuwa Palastina, akitumia lugha yake ya kawaida ya mafumbo, kuhusu safari hii? Aliwaambia:

"Itakuwa kama mtu anayeondoka nyumbani kwenda safari akiwaachia watumishi wake madaraka, kila mmoja na kazi yake Ninayowaambieni ninyi, nawaambia wote: Muwe macho" (Marko 13:34-37; Luka 19:12).

UGUNDUZI KUTOKA KITUO CHA WABUDHA CHA HIMIS NCHINI LADDAKH

Hapo mwaka 1887 msafiri mmoja wa Kirusi aitwaye Nicholas Notovitch, alizuru kituo kimoja cha wafiasi wa dini ya Budha katika sehemu moja ya nchi ya Himalaya iitwayo Laddakh (India). Kule mguu wake uliovunjika ukawa kisababu cha ugunduzi wa kiajabu. Yeye asema:

Nilipokuwa safarini huko Leh, mji mkuu wa Laddakh, nilizuru Himis, kituo kikubwa (cha Wabudha) kilichokuwa katika vitongoji vya jiji hilo". Kule, kwa msaada wa mkalimani wangu aliyetafsiri toka lugha ya Kitibeti nilinakili kwa ungalifuaya kama zilivuosomwa na Lama" kufuatana nazo, "Wakati Isa (yaani, Yesu) alipofikia umri wa miaka 13, ambapo Mwisraeli aliwajibika kuoa mke ... Isa aliacha nyumba ya baba yake kwasiri, akaitoka Jerusalem na akajiunga na msafara wa wafanyi biashara alisafiri kuelekea Sindh (ambayo sasa ni sehemu ya nchi ya Pakistan)" ili ajiimarishe katika neno la Mungu na kujifunza sheria ya mtukufu Budha. Kwa miaka sita alitembelea miji mitakatifu mbalimbali ya India. Makuhani wa Kibaniyani (waitwao Mabrahmin) wakatokea kuwa maadui zake (kumbuka: Mtakatifu Tomaso aliuawa na Mabrahimin hao mjini Madras, India).

"Lakini Isa aliyepashwa habari ya njama zao na Mashudra (ambao Mabaniyani hata hawawagusi eti kwa sababu ya unajisi wao) akatoroka usiku kutoka Jaggermaut hadi mahali alipozaliwa Mtukufu Budha. Miaka sita nyumaye akaondoka Nepal na milima ya Himalaya akateremka katika bonde la Rajputana (huko huko India) na kaelekea magharibi, akiwahubiria watu mbali mbali".

"Isa alipowasili Palastina alizunguka hapa na pale akiimarisha ushujaa wa Waisraeli kwa neno la Mungu na maelfu walimfuata kusikia mafundisho yake".

"Lakini watawala wa mji wakamuogopa na wakamshitaki kwa Pilato, Gavana wa Yerusalem, aliyeamuru ya kwamba Isa akamatwe Kisha Isa akaletwa toka gerezani na akakalishwa mbele ya Gavana baina ya wezi wawili". Habari hizi zamalizia kwa kusema Isa alisulubawa na kuzikwa na baada ya siku tatu malaika wakayachukua mabaki yake. (Notovitch: Vie Incomme de Jesus Christ, Paris, 1894, yaani Maisha yasiyojulikana ya Yesu Kristo).

(Kumbuka: Kabla hatujaendelea mbele, ni lazima kudhihirisha ya kuwa ugunduzi huu uliwapunja waandishi wengi wakakimbilia uamuzi eti Yesu kwa kweli alipitisha miaka yake isiyojulikana (tokea mwaka wa 13 hadi mwaka wa 29) akajifunza katika nchi za Himalaya. Sasa hivi tutauzungumzia ugunduzi huu muhimu. Lakini kwanza na tumalizie habari za Notovitch.)

Wakati Notovitch alipozipanga habari zake "ili zitangazwe" alizikabidhi kwa Monseigneur Platon, Askofu Mkuu wa Kiev, azisahibishe. Yeye ijapo aliamini umuhimu wa ugunduzi huu, alimshawishi Notovitch kutozitangaza habari hizi, akidokeza ya kuwa jambo hili lingekuwa kinyume na faraja ya huyo mwandishi. Askofu huyo hakutoa sababu zozote. Mwaka mmoja baadaye alipokuwa mjini Roma, alimkabidhi maandiko hayo yake Kadinali mmoja aliyeheshimika machoni pa Baba Mtakatifu. "Kwa nini umelazimika kuzipigisha chapa habari hizi? Kadinali huyo akazidi kusema: "Hakuna mtu anayezithamini; na jambo hili litakuletea maadui wasiohesabika; NA UKIWA WAHITAJI PESA NAWEZA KUKUPA kuficha maandiko yako haya." Notovitch alionyesha sehemu ya mpango wake kwa Kadinali Rotelli, ambaye hakuonana naye mjini Kastantina. Huyu pia alipinga utangazaji wa habari zenyewe. Akaongeza kusema: "KANISA LINADHURIKA SANA NA MFULULIZO HUU MPYA WA MAWAZO YA KIKAFIRI:

NAWE UTAWAPA SILAHA MPYA WALE WASINGIZIAJI WA ITIKADI ZA INJILI" (J.D Shams: "WHERE DID JESUS DIE?", kilichotolewa na Baker & Witt London, 1945, uk. 157, habari iliyofupishwa toka "THE UNKNOWN LIFE OF JESUS CHRIST" tafsiri ya Lovanger, uk. 8-12.

Lakini hongo ya Kadinali haikufaulu wala matisho yake. Notovich hatimaye alifafulu kuzipigisha chapa habari alizokuwa amezipanga. Upesi upesi kitabu hicho kilipigishwa chapa mara sita na nakala zake zote zikauzwa haraka. Tafsiri zake za Kiingereza pia zilitolewa na zote, zikanunuliwa. Zipo nakala mbili za tafsri hiyo katika jumba la Mambo ya Kale (la British Museum). (i. Alexina Loranger: "THE UNKNOWN LIFE OF JESUS CHRIST", kilichotolewa na rand MacNally & Co. Chicago, New York, 1894 na ii. Violett Crisp, London, Hutchinson & Co.

Bi Henrietta Merick, akiwa na nia ya kuhakikisha habari za Notovitch, mwenyewe akafunga safari hiyo ngumu hadi kituo cha Himis na akathibitisha maneno ya Notovitch katika kitabu alichotunga Bi Merick. Hicho nacho kikatangazwa (Henrietta Merrick: "IN THE WORLD ATTIC", Roerich Museum Press, New York 1929.

Mvumbuzi mwengine, kwa jina Nicholas Roerich, alifanya utafiti wake peke yake na akatangaza habari zake kutoka huko New York, Marekani. (Nicholas Roerich: "THE HEART OF ASIA" Roerich Museum Press, New York 1929).

Sasa kumeandikwa vitabu na makala kadha wa kadha kulihusu jambo hili na kuhusu ule mlingano wa Ukristo na dini ya Budha. Uchunguzi zaidi ungali umo mbioni. Kisa cha ziara ya Yesu pande za Mashariki na Kaskazini mashariki chajulikana kwa watu wengi.

MAONI YA WAISLAM WAAHMADIYYA KUHUSU UGUNDUZI HUU WA NOTOVITCH

Visa vinavyoenea sana havikosi mwanzo wake. Hii siyo kusema kila kisa huwa ni kweli tupu. Haielekei kamwe wala kukubalika ya kwamba kijana wa umri mdogo kama miaka 13 angethubutu kufunga safari ya maili elfu nyingi mbali kutoka kwao, tena iliyojaa hatari nyingi, ili kujifunza maamrisho ya dini asiyojua katika siku hizi.

Badala ya kuuita ugunduzi huu eti "Mfululizo mpya wa Mawazo ya Kikafiri", ambayo si rai ya busara, ni lazima tutafute kile kilichowafanya waandishi hao wa Kibudha kumjulisha Yesu katika shughuli zao, na kumshusha cheo wakimfanya mwanafunzi wa Budha.

Rai ya Waislam Waahmadiyya iliyowasilishwa na hayatı maulana Jalal-ud-din Shams, aliyekuwa Mbashiri mkuu huko mashariki ya Kati na Uingereza na Imamu wa Msikiti wa Jumuiya ya Ahmadiyya mjini London, kuhusu jambo hili ni kwamba:

"Kama Yesu hakuenda India, basi hapo hakungekuwa na sababu iwayo yoyote kwa waandishi wa Kibudha kutaja mahubiri yake kule. Kwa upande mmoja wao hawakuthubutu kutoutaja ukweli kwamba Yesu alihubiri pande zile, Ilhali kwa upande mwingine walitambua ubora wa mafundisho yake kuliko mafundisho ya Budha na ya Mabrahmani. Kwa hivyo wao walivunga habari hivi makusudi ili kuonyesha utukufu wa Gautama Budha, na badala ya kusema wazi wazi ya kwamba Yesu aliizuru Bara Hindi hali yu nabii wa Mwenyezi Mungu, na kwamba mafundisho hayo yalikuwa yake hasa, wakayahesabu kuwa mafundisho ya Budha huku wakidai eti Yesu alifika India, akiwa chipukizi, ili kuepa ndoa na ili apate mafunzo ya dini" (J.D Shams: "WHERE DID JESUS DIE?", kilichotolewa na Baker &Witt London, 1945, uk. 157, habari iliyofoipishwa toka "THE UNKNOWN LIFE OF JESUS CHRIST" tafsiri ya Lovanger, uk. 8-12).

Kur'ani Tukufu inamtaja Yesu (Isa) kuwa Nabii Mtumishi wa Mungu. Kulingana na mafundisho ya Kur'ani Tukufu, Yesu alisema:

.... Hakika mimi ni mtumishi wa Mwenyezi Mungu; Amenipa Kitabu na Amenifanya Nabii. Na amenifanya mbarikiwa popote nilipo" (Kur'ani Tukufu 19:31, 32). Twamalizia kwa kusema ya kwamba Yesu alikwenda India, na sehemu zingine za majimbo ya Himalaya baada ya kusulubiwa na wala siyo kabla ya tukio la msalaba. Yeye alikuja kufundisha, wala siyo kujifunza. Hapa wafuasi walikuwa wengi lakini hawakuitwa Wakristo; kwa maana wao kamwe hawakufunzwa "eti Yesu alifia dhambi zetu". Walimkuta mzima baada ya kutolewa msalabani!

UGUNDUZI KUTOKA KITABU CHA BHAVISHA MAHA PURANA

Bhavisha Maha Purana nikitabu cha Mabaniyani kilichoandikwa kwa lugha ya kale iitwayo Sanskrit, kwenye mwaka wa 3191 zama za Laukika, ambao walingana na mwaka wa AD 115. Hii ina maana ya kuwa kitabu hicho kiliandikwa karibu wakati sawa na Injili ya Yohane. Maandiko yake ya asili bado hayajagundiwa.

Kitabu hiki kwanza kilifasiriwa na kuandikwa katika lugha ya Kihindi ya siku hizi mnamo mwaka wa 1910, kwa amri ya mtawala wa Kashmir, na kikasababisha ugunduzi ya kwamba Yesu alikutana na Mfalme Shaliwahin wa India mahali paitwapo Voyen, karibu na Srinagar, Mji mkuu wa Kashmir. Habari ya mkutano huo imeandikwa ndani ya Bhavisha Maha Purana. Hapa chini twanukuu sehemu yake baada ya kuifupisha:

"Siku moja Mfalme Shaliwahin alifika nchi ya Himalaya. Kule alimuona mtu mtukufu wa Saka huko Voyen. Alikuwa mweupe wa rangi na alivalia mavazi meupe. Mfalme akamwuliza, "Wewe

u nani?" Akasema, "Mimi ni YUS ASHAFAT na NIMEZAWA NA BIKIRA." Mfalme alipoyastaajabia, yeye akaongeza, "Nimekwambia kweli. Nimekuja kuitakasa dini ambayo ilianza nchi za mbali" Mfalme akauliza, "Dini yako ni ipi?" Akasema, "Ewe mfalme! pale ukweli ulipopotea na hulka njema kuangamia, HAPO MIMI NIKADHIHIRI MIONGONI MWAO KAMA MASHIHA" Katika jitihada zangu pale wenyе dhambi na wadhalimu walipotaabika, MIMI PIA NIKATAABISHWA KWA MIKONO YAO". Yule mfalme akamwomba aelezee dini yake. Akasema, "Dini yangu ni upendo, usafi wa moyo na fikira, na ukweli. Mwanadamu yampsа kumwabudu Mungu, Aliye asili ya jua la mbinguni na Anayevivutia viumbe vyote". Kisha mfalme akatoa heshima zake na akaondoka. ("BAVISHA MAHA PURANA", uk. 3, mlango 2, kifungu cha 21-31. Kilipigwa chapa mara ya kwanza, 1910. Fungu hili limefasiriwa kwa Kiingereza na Profesa Kosambi wa Tata Institute of Fundamental Research, Bombay, India. Vilevile someni "JESUS IN ROME" cha Robert Graves kilichotolewa na Casell & Co. Ltd., London uk. 76-79.

Hapa jina la huyu MZAWA WA BIKIRA limetajwa kuwa ni YUS ASHAFAT. Hii ni karibu sana na YUSU ASF, jina la Kiyahudi, maana yake "YESU MKUSANYAJI"; kwani alikuja kwa kukusanya kondoo zake waliopotea wa nyumba ya Israeli.

Kwa kufuatia hesabu kufika enzi ya Mfalme, Shaliwahin, ambaye alianzisha majira yake mwenyewe yaitwayo "Majira ya Shaliwahin" mkutano huo wa Voyen ulikuwa katika mwaka wa AD 78. Umri wa Yesu wakati ule ni lazima uwe ulikuwa umekiuka miaka 85. (Andreas Faber Kaiser: "JESUS DIED IN KASHMIR" kilichotolewa na Gordon & Cremonesi, London, 1977, uk. 111-118).

MAANDIKO YALICHONGWA PENYE UKUMBUSHO WA TAKHT-E-SULEIMAN

Pembezoni mwa ziwa liitwalo Dal lilizungukwa na mandhari ya kupendeza karibu na mji wa Srinagar. Pale; pamejengwa ukumbusho wa kale sana uitwao “Takht-e-Suleiman” (yaani Kiti cha Enzi cha Nabii Suleiman). Kulingana na maoni ya Waisraeli wa Kashmir, ukumbusho huo ni nakala hasa ya kiti cha Enzi cha Suleiman, kilichovunjwa na mfalme wa Babeli, Nebukadnezari (Bukhtnassari). Kuuhusu ukumbusho huo mwana historia mashuhuri wa huko Kashmir aitwaye Mulla Nadir, ameandika hivi:

“Kilelenimwamlima Suleiman ulikuwe poukumbusho uliokuwa na kuba, nao ulichakaa. Mfalme wa pale, akampa Mwajemi mmoja aitwaye Suleiman, aliye kuwa mmoja wa mawaziri wake, kandarasi ya kuufanya, ukumbusho huo marekebisho. Mabaniyani wakapinga wakidai ya kwamba mtu huyu alikuwa mgeni (wala si mwananchi). Karibu na wakati huo Mtukufu Yus Asaph, kutoka Palastina, aliwasili katika bonde takatifu. Yeye akadai kuwa yu Nabii na kaeneza mahubiri yake. Kwa vile idadi kubwa ya wenyehi wa nchi ya Kashmiri walikuwa wafuasi wake, mfalme Gopadatta aliuwasilisha kwake ule upinzani wa Mabaniyani. Kwa kufuatia mapendelekezo ya Yus Asaph, mtu huyu Suleiman, ambaye Mabaniyani walimuita jina Sandeman akafanya kazi ya kuurekebisha ukumbusho; na akachonga maandiko (yafuatayo) katika mojawapo wa ngazi zake:

“Wakati huu Yus Asaf anatangaza unabii wake. Mwaka wa 54.”

Na juu ya ngazi nyingine, akaandika: “Yeye ni Yesu, Nabii wa mwana wa Israeli. (TAARIKH - E- KASHMIR - cha Mulla Nadir, uk. 69). (Muswada wa Kiajemi haujagunduliwa bado). Kwa maelezo zaidi, someni: “TAARIKH-e-KASHMIR” cha Hassan, jalada 3, uk. 25 na (2) Research Library Srinagar.

Kumbuka: Sehemu ya maandiko hayo katika lugha ya Kiajemi yaweza kuonekana mpaka leo.

C. YESU ALIFIA KASHMIR

UGUNDUZI WA KABURI LA YESU (NABII ISA) A.S.

"Kwa kawaida hilo linajulikana kuwa ni Kaburi la Nabii Alikuwa mwana wa mfalme aliyekuja toka nchi ya mbali. Alikuwa mkamilifu katika utawa, ucha - Mungu na ibada. Mwenyezi Mungu Alimpa Unabii, na akashughulika katika kuwahubiri watu wa Kashmir. Jina lake lilikuwa Yus Asaph." (Taarikh-e-A'zami, uk. 82).

Haya yaliandikwa na mwana - historia mmoja, karne mbili na nusu zilizopita. (Khawaja M. Azam Didama: "TAARIKH-e-A'ZAMI" Muswada wa 1729, uliopigwa chapa mwaka wa 1884, Lahore Pakistan, uk. 82).

Kaburi hilo lipo kando ya ziwa mashuhuri liitwalo Dal, ndani ya Sri Nagar, mji mkuu wa Kashmir. Huenda kwa sababu ya kuwa mahala pa Yus Asaf, Sri Nagar pakapanuka kama palivyo leo. Zipo sehemu nydingine kadhaa nchini Kashmir ambazo pia zimeambatanishwa na jina lake, kwa mfano "Yus Marg" (Nyika za Yus Asaf); "Aish-Muqaam" (Mahali aliposhukia na kupumzika) n.k. Kwahivyo, kuingia kwa Yus Asaph nchini Kashmir kumeacha alama za kudumu juu ya uso wa nchi hiyo. Na kwa nini isiwe hivyo, ilihali yeye aliishi hapo kama "Mwana-Mfalme" na akiwa "Nabii." wananchi wote wakashika dini yake.

Jengo lenyewe ni la mtindo wa Kiyahudi na Kaburi limo ndani yake, likiwa limeelekezwa upande wa mashariki-magharibi sawa na desturi za maziko ya Waembrania. Kaburi hilo daima lilikuwa mahali patakatifu palipofanyiwa ziara na watu wakubwa kwa wadogo.

Kugunduliwa kwake

Kaburi hili lilikuwepo kwa muda mrefu; lakini ni mwanzilishi wa Jumuiya ya Waislam Waahmadiyya aliyetangaza ugunduzi wa kaburi hili katika zama hizi zetu, na kuhakikisha kwamba

kweli ni kaburi la Yesu (Nabii Isa), mwana wa Mariam; na ya kwamba Yesu ndiye aliye akiitwa Yus Asaf zama hizo. Habari zaidi kumhusu Yus Asaf ni kama ifuatavyo:

(A) "Alizunguka katika nchi na miji mbalimbali mpaka akaifikia nchi iitwayo Kashmir. Alitembea na akaishi na kukaa nchini humo mpaka kufa kwake. Akaacha nyuma mabaki ya mwili (wa udongo) na akapanda kwenye nuru. Kabla hajafa alimwita mwanafunzi wake, kwa jina Yabadna akampa wasia huu: "Kuondoka kwangu toka Ulimwengu huu kumewadia; zingatia wajibu wala usitetereke hata kidogo kutoka njia ya ukweli, na ukatii sheria zote" Halafu akamsihi mwanafunzi huyo amfanyie kaburi lake pale atakapofia. Kisha alielekeza miguu yake upande wa magharibi na kichwa chake upande wa mashariki, na akakata roho." (Ikmaluddin, uk 357, 358).

Kitabu hiki "Ikmaluddin" kinathaminiwa sana; kwa maana kinatoa habari za kale sana ambazo zimewahi kuandikwa hata hivi leo kumhusu Yesu Kristo (Yus Asaf wa zama hizo). Hivi sasa kitabu hiki kina zaidi ya miaka elfu moja. Maneno yafuatayo yadokeza jinsi kitabu hiki (na mwandishi wake) kionekanavyo mbele ya macho ya watu wa Magharibi:

"Mwandishi mashuhuri wa pande za Mashariki ambaye pia alijulikana kwa jina la Sheikh As-Sa'id-us-Sadiq, aliyefia huko Khurasan katika mwaka wa 962 AD, aelezea safari za Yus Asaf, ndani ya kitabu chake mahsusisi Ikmaluddin. Kitabu hiki kinacho thaminiwa mno na wataalamu wa Magharibi juu ya habari za Mashariki, baadaye kilifasiriwa katika lugha ya Kijerumani na Profesa Muller wa Chuo Kikuu cha Heidelberg. Mwandishi wa kitabu hiki, alisafiri sana ili kukusanya habari za kitabu chake, ambacho dhati yake ni kweli tupu." (Andreas Faber Kaiser: "JESUS DIED IN KASHMIR" kilichotolewa na Gordon & Cremonesi, London, 1977, uk. 96).

Kitabu hiki Ikmaluddin, hakituelezei kwa maneno ya kinaganaga, huyu Yus Asaf alikuwa nani. Walakini mwandishi wake anagusia ukweli wa kimsingi ya kwamba Yus' Asaf

alikuwa "akilinganisha mti wa BUSHRA aliyohubiria watu, na chemchem ya maji aliifananisha na elimu na maarifa aliyogaaliwa, ilhali watu waliomzunguka na kuingia dini aliwafananisha na ndege.

Katika lugha ya Kiebrania BASHORA (au BUSHRA kwa kiarabu) maana yake ni HABARI NJEMA; kwa hiyo si vigumu kwetu sisi kukisia ni nini ambacho Yus Asaf angewafundisha wafuasi wake wa pande hizo za mashariki. (Kwa Kiyunani, BASHORA ni INJILI na tafsiri ya Injili kwa Kiswahili iliyotangazwa na Muungano wa Vyama vya Biblia (UBS) huku Afrika ya Mashariki mnamo mwaka wa 1977, yaitwa pia HABARI NJEMA (kwa watu wote) ambayo ni tafsiri sahihi ya BUSHRA; Mfasiri).

(B) Yus Asaf aliwafundisha watu akitumia maneno yaliyojaa mifano. Kitabu cha Yus Asaf kina mifano ifuatayo: "Mpanzi apandapo mbegu zake, zingine huangukia njiani zikakanyagwa na mpita njia. Zingine huliwa na ndege, na mbegu zingine kuanguka juu ya ardhi yenye miamba Mpanzi ndiye mtaalamu na mbegu ni hekima yake. Mbegu ziangukazo njiani ni ile hekima iingiayo katika sikio hili na kutoka katika sikio lile, mara. Neno la hekima liangukalo juu ya ardhi yenye miamba ni lile lisilozingatiwa kabisa. Na mbegu zimeazo kati ya miiba ndiyo maneno ya hekima yenye kupingwa vikali na nafsi ya mtu. Na zile mbegu ziangukazo katika ardhi nzuri ndizo zenye kuingia moyoni, hutoa mizizi na kazaa matunda (K.S. Mackdonald: "STORY OF BARLAAM AND JOSAPHAT", kilichotolewa na Thacker S. Pinl & Co., Calcutta, uk. CXI).

Twalinganisha haya na maneno ya Mathayo 13:3; Marko 4:3 na Luka 8:5.

Kitabu hicho kina mifano mingine mingei. Kilifasiriwa karibu katika lugha zote za Ulaya. Itakumbukwa ya kwamba kundi moja la Wakristo lamheshimu sana Yus Asaf hata lipo kanisa moja nchini Silsila lililojengwa kwa mintarafu ya jina lake. ("REVEU DU MONDE MUSULMAN"), jalada la kwanza,

Nambari 4, Februari 1907 uk 533-576 katangazwa tena: "A SHORT SKETCH OF AHMADIYYA MOVEMENT IN ISLAM", lililotolewa na Ahmadiyya Mission, P.O. Box 418, Lagos, Nigeria.

Mwishoni, Joseph Jacobs asema kuambatana na habari ya kale sana ya huyu Yus Asaf, ya kwamba hatimaye alifika Kashmir alikofia. (K. S. Mackdonald: "STORY OF BARLAAM AND JOSAPHAT", kilichotolewa na Thacker S. Pink & Co., Calcutta, uk.CV).

C. Mlinzi wa kaburi hilo anayo hukumu iliyotolewa miaka 200 iliyopita na kutiwa sahihi na mahakimu (Mamufti) watano wa mijini Sri Nagar. Hukumu hiyo ilitolewa ili kuamua ubishi kuihusu haki ya ulinzi wa kaburi lile. Sehemu ya hukumu hiyo ni kama ifuatavyo:

"Baada ya kuthibitisha ushahidi iligunduliwa ya kwamba katika enzi ya mfalme Mhindu Gopadatta, aliyelirekebisha jengo la mlima Suleman na akajenga mahekalu mengi, mtu aitwaye Yus Asaf alikuja. Alikuwa mwana wa kifalme Haya yalitendeka baada ya gharika kubwa ya Kashmir wakati watu walipopotoka na kuabudu masanamu. Yus Asaf aliletwa kama Nabii kuwahubiria watu wa Kashmir. ALIHUBIRI UMOJA WA MWENYEZI MUNGU MPAKA MAUTI YALIPOMFIKIA NAYE AKAFA. Alizikwa kule katika mtaa wa Khanyar pembezoni mwa ziwa katika mahali pajulikanapo kama "Rauzabal" Kwa vile ambavyo mahali pale hujiwa na watu wote, wakubwa kwa wadogo, na mtu aliyetajwa kabla Rahman Mir ndiye mrithi wa usimamizi wa pale, ye ye anapewa mamlaka ya kupokea sadaka zinazotolewa pale" Imetolewa chini ya mkono wetu siku hii ya kumi na moja ya Jamada-al-Thaniya 1184 Hijiriyya.

Imesahihiva na kutiwa muhuri na Mulla Fazal, Hakimu Mkuu wa mahakimu wengine wanen. (Andreas Faber Kaiser: "JESUS DIED IN KASHMIR" kilichotolewa na Gordon & Cremonesi, London, 1977, uk. 104, 105).

Mafundisho ya umoja wa Mwenyezi Mungu yaashiria kwamba yeeye alikuwa Nabii wa Mungu aliyetokana na ukoo wa Israeli. Kwani katika Ulimwengu huu wetu ni Biblia na Kur'ani vinyavyotoa fundisho hili. Lakini Kur'ani Tukufu haikuwepo katika enzi ya mfalme wa Kibaniyani Gopadatta, iliyoanzia kwenye mwaka wa AD 49. Kur'ani Tukufu iliteremshwa miaka mia sita baadaye.

Kadhalika hadithi za watu wa Kashmir zinazosimuliwa hadi leo, ni ushahidi wa maana. Ukiwaliza kulihusu kaburi lile, watasema: "Ni kaburi la Nabii Sahib" au "Shahzada Nabii" au Hadhrat Yus Asaf" wakiwa na maana ya kuwa mwenye kuzikwa pale ni Nabii, au Nabii aliyekuwa mwana wa kifalme, au Mtakatifu "Yus Asaf". Nao husema alikuja toka upande wa magharibi, zamani za kale.

Kwa ufupi

Ushahidi wote uliopo ukiunganishwa ya kuwa lile kaburi la Sri Nagar karibu na ziwa Dal, ni kaburi la Yus Asaf, aliyekuwa nabii wa Mwenyezi Mungu na alikuwa mwana mfalme, mtimilifu wa utawa na ucha - Mungu, ambaye aliwafunza watu kwa mifano na akakiita kitabu chake BUSHRA (yaani, Injili) alitokea pande za magharibi nyakati za utawala wa Gopadatta. Alikuwa Mhebrania, aliywafunza watu Umoja wa Mwenyezi Mungu, na alipo fariki alizikwa kukingama upande wa mashariki na magharibi, kuambatana na desturi za Wahebrania.

LAKINI

Halikuwa jambo jingine ambalo wana-historia na waandishi wa habari za Yus Asaf walilolifahamu kulihusu kaburi hilo isipokuwa ukweli kwamba hilo lilikuwa kaburi la Yus Asaf, na kwamba watu wa Kashmir waliendelea kulizuru kama walivyofanya tangu zamani. Si zaidi ya hapo. Ingawa watu wa

Kashmir karibu wote ni Waislam, lakini wao pia kama Waislam wengine wa India na kwingineko walibaki katika hali ya upotofu kuhusu ukweli ya kwamba Yesu, mwana wa Mariamu, ambaye Kur'ani Tukufu imemtaja kama Masiha na Nabii (wa mwisho) toka nyumba ya Israeli, ndiye aliyezikwa katika kaburi lile.

Hivyo, watu wa ulimwengu huu walikuwa na macho yao kuonea, lakini hawakutambua. Ilikuwa ni katika hali kama hii ambapo Sayyidna AHMAD wa Qadian, India, alipodhihiri kama Masiha wa zama hizi naye akayafumbua macho ya walimwengu na kuondoa upofu wao. Kisha akawaonyesha mahali pale mwana wa Mariam alipopumzika kwa amani. Akatangaza ukweli ya kwamba yeze mwana wa Mariam kamwe haishi mbinguni wala hatashuka toka kule akiwa na mwili wake wa udongo, kuja kuuhukumu ulimwengu huu, au kuzusha vita vya "Jihad" dhidi ya makafiri, kama walivyoamini Waislam wengine (isipokuwa Waislam Waahmadiyya). Kosa la Wakristo waliodhani kutakuwa na vita halisi (Armageddon) baina ya Iblisi (Joka kuu) na baina ya wafuasi wa kweli wa Masiha lilielezwa wazi. Haya ni mambo ya kiroho, akaeleza Sayyidna Ahmad a. s., wala haikuwa kazi ya Masiha kumwaga damu za wanadamu.

ATHARI YA UVUMBUZI HUU

Uvumbuzi huu ulifanyika katika mwaka 1895. Mara tu baada ya kutangazwa, ukaamsha chuki na kutoamini mionganini mwa Waislamu na Wakristo pia. Lakini mwamko mwingine uliwaamsha wageni, watalii na wapelelezi waliomiminika toka pembe zote za dunia ili kuona vile kaburi hilo lilivyo. Hamu ya wengine ilikuwa kudadisi tu; lakini mionganini mwao walikuwemo watafutao ukweli.

ZIARA, MAONI NA UFAFANUZI

Haiwezekani kuandika majina ya watu wote waliolizuru kaburi hilo. Wala hatutamudu kamwe kunukuu hapa chini maoni yao wote. Kwani idadi yao ni kubwa na inazidi kuongezeka kila siku. Tumechagua haya yafuatayo:

(a) Mwaka wa 1903 ilikuwa zamu ya padre Weitbrecht.

Alifika kuliona kaburi baada ya kuipokea habari ya ugunduzi wake. Yeye alivutika. Aliandika katika gazeti la Kikristo (lililoitwa "EPIPHANY") kuwa yeye alikubali ya kwamba kweli kaburi hilo likuwa la Yus Asaf, lakini halimhusu Yesu. (J.D Shams: "WHERE DID JESUS DIE?", kilichotolewa na Baker & Witt London, 1945, uk. 171, 172. Pia tazama, hashiya (a) habari iliyofupishwa toka "THE UNKNOWN LIFE OF JESUS CHRIST" tafsiri ya Lovanger, uk. 8-12).

Hata hivyo, ziara yake ndicho kitu cha maana. Bila shaka alilingwiwa na wasiwasi juu ya uhai wa Yesu Kristo. Alilizuru kaburi lile ili kutosheleza udadisi wake.

(b) Katika mwaka wa 1909 ikawa zamu ya Sir Francis Younghusband, mwakilishi wa kisiasa huko Chitral ambaye wakati ule alikuwa balozi wa Uingereza nchini Tibet, na kabla ya hapo alipata kufanywa balozi wa Malkia katika Kashmir. Alipopashwa habari zilizotangazwa na Sayyidna Ahmad a.s. wa Qadian, alifunga safari kulizuru kaburi hilo. Na baadaye akaandika akisema:

"Mtakatifu mmoja aliyeitwa Yus Asaf aliishi huko Kashmir kama miaka 1900 iliyopita. Yeye alihubiri akitumia mifano; na mingi katika hiyo ilikuwa ileile iliyotumiwa na Yesu, kama ule mfano wa Mpanzi. Kaburi lake liko huko Sri Nagar. Rai ya mwanzilishi wa Twarika ya Qadiani ni hii kwamba Yus Asaf ndiye Yesu. (Sir Francis Younghusband: "KASHMIR", Black, London, 1909, uk. 129, 130).

(c) Katika kitabu chake cha mwaka wa 1920, kiitwacho "If

Jesus Did Not Die On The Cross" (yaani, Endapo Yesu Hakufa Msalabani), Hakimu mmoja wa Uzunguni Sydney, Australia, aliandika:

"Yanibidi niseme tena ya kwamba hatujui. Huenda ikawa baada ya kuhubiria makabila yaliyopotea ya Nyumba ya Israeli, katika nchi zile za mbali, Yesu alifia Sri Nagar, na akazikwa katika kaburi lile ambalo sasa lajulikana kwa jina lake (Ernest B. Docker: "IF JESUS DID NOT DIE ON THE CROSS", kilichotolewa na Robert Scott, London 1920, uk. 71).

(d) Mgeni mwingine alikuwa John Noel, mwandishi Mmarekani. Alitembelea Kashmir mnamo mwaka wa 1930, kisha akaandika akisema:

"Wazalendo wa Kashmir ... wana sura asili ya Kiyahudi kuliko Myahudi ye yeyote uliyewahi kumuona mlingano wa kustaa jabisha - au, kweli ni mlingano? - ni ya kwamba zipo hadithi thabiti kule Kashmir za wazalendo hao kuhusiana na Mayahudi pana uvumi ya kwamba kwa kweli Yesu kamwe hakufia msalabani, bali alishushwa toka msalabani naye akatoweka kuyatafuta makabila yaliyopotea, na ya kuwa alifika Kashmir, Laddakh na Tibet ndogo, akafa na akazikwa kule Sri Nagar". (Jarida "ASIA", U.S.A. toleo la Oktoba 1930, chini ya kichwa cha maneno: "THE HEAVENLY HIGH SNOW").

(e) Katika mwaka wa 1939, Ahmad Aslam alimwandikia mhariri wa gazeti la "Sunrise", Lahore, India (sasa Pakistan) kama ifuatavyo;

"Nilimtajia Khanyar yule mwendeshaji wa gari la farasi, akanijibu kwa shauku kubwa, "Bwana, wataka kuliona kaburi la Nabii Sahib?" Nikasema, Naam. Mara tukaelekea kule Nilifahamishwa kwamba wageni wa aina nydingi, toka nchi ya India na nchi za mbali, walifika kuliona kaburi lile. Hata mjumbe wa mfalme wa Uingereza alifika hapa. Mimi nilipata kiherehere niliposikia hayo na nikauliza kwa hima; NI MJUMBE YUPI WA MFALME UNAYESEMA?" Sina hakika bwana lakini

ni yule ambaye alikuwa na mkono mmoja tu." "Bila shaka huyo alikuwa Lord Halifax, Waziri wa Uingereza wa nchi za kigeni ambaye wakati uleule pia aliitwa Lord Irwin. Ziara ya Lord Halifax haikutangazwa magazetini. Kwa vyovyote, mimi sikumbuki kama niliwahi kusoma habari hizo popote. Wala hapana awezaye kujua sababu iliyomfanya Lord Halifax kuja kuutuliza moyo wake kwa njia ya siri". ("THE SUNRISE", jalada 10, nambari 16, Aprili 22, 1939, Lahore, Pakistan.

(f) "KWA NINI KABURI HILO LISIFUKULIWE?"

Ndilo swalii liloulizwa na gazeti la 'Wimbledon Borough News' London, katika matoleo yake ya mwezi wa Machi 1, 8 na 29, mwaka wa 1946. Katika mwaka huohuo gazeti jingine la huko London liliandika likisema;

"Hapa katika mtaa wa Khanyar, mjini Sri Nagar, Kashmir pana kaburi ambalo Waislamu wanaamini kuwa ni la Yesu. WANATAKA LICHUNGUZWE" (Psychic News, Aprili 20, 1946).

(g) Mtaalamu mmoja wa Kijerumani, Andreas Faber Kaiser, alipata fursa yake mnamo mwaka wa 1976, na akaandika;

"Nilisikia uvumi ya kwamba Yesu hakufia msalabani na ya kuwa alikimbilia pande za mashariki ambako yumkini alizikwa na moyo wangu haukuathirika sana mpaka nilipopashwa habari za kuwepo kwa picha moja nchini Hispania inayoonyesha kaburi linalosifika la Yesu huko Kashmir.

Nilipopata nakala ya picha hiyo, nikaanza shughuli za kukusanya dalili zihusikanazo. Nikiwa katika kushughulikia jambo hili rafiki yangu mmoja alinionyesha makala katika gazeti moja la Ujerumani liitwalo "STERN" yaliyozungumzia habari za kutoroka kwa Yesu na kufika kwake nchini Kashmir

Nilimwarifu mwandishi wa makala hayo, Klaus Liedtke, katika afisi ya gazeti hilo STERN, mjini Yew York, Marekani kwamba

nataka kujua mengi zaidi kuhusu shauri hili. Nilizungumza na mpiga picha, Jay Ullal, katika ofisi ya gazeti hilo mjini Hamburg. Kwa huruma kubwa, hao wawili walinitumia maelezo yote waliyokuwa nayo juu ya habari hii. Hii ndiyo ikawa sababu ya mimi kujuana na Waislamu Waahmadiyya waliokuwa Ujerumani, na pia makao yao makuu nchini Pakistan Baada ya kutembelea Kashmir na kuyachunguza maandishi, masimulizi ya watu na kaburi lenyewe ni maoni yangu ya kwamba habari za safari mbili za Yesu za India na Kashmir, habari za kufia na kuzikwa kwake nchini kule pana uwezakano mkubwa kwamba ni kweli. Uthibitisho wa waziwazi haupo, na kwahivyo mimi naamini ya kuwa yale makaburi² yahusikayo itabidi yafukuliwe ili yachunguzwe kwa mbinu za kisayansi. Zaidi ya haya ningependa kupendekeza kuanzishwa halmashauri ya kimataifa wakiwemo wataalam wa Biblia, wataalam wa lugha, wataalam wa historia ya pande za mashariki na wanachuoni wa Kiislam ili waweze kufanya uchunguzi na kutafuta ukweli ulipo, juu ya misingi ya kisayansi" (Andreas Faber Kaiser: "JESUS DIED IN KASHMIR" kilichotolewa na Gordon & Cremonesi, London, 1977, uk. 160-166).

(h) Isitoshe, tunazo makala chungu nzima katika mijala na magazeti. Miongoni mwa zile za hivi majuzi tunazo makala kama:

Jarida liitwalo: Illustrated Weekly of India, lililotoa makala "Is Jesus Buried in Kashmir?" (yaani je, Yesu amezikwa Kashmir?), katika toleo lake la mwezi Aprili, 1972.

²Anaashiria kaburi jingine, analolidhania kuwa ni la Nabii Mussa A.S. Bwana Andress Faber Kaiser anataka makaburi yote mawili yachunguzwe. Lakini kulihusu kaburi lile jingine maoni ya Waislamu ni kwamba lipo karibu na mipaka ya Palastina, kama alivyoonyeshwa Mtukufu Muhammad s.a.w. katika njozi. (Naam, yawezekana ya kwamba wana wa Israeli walipohama Palastina walichukua mifupa michache ya Nabii Mussa a.s. kwa kupata baraka zake, walipokuja nchi ya Kashmir wakaizika pale na kujenga juu yake. Mfasiri).

Jarida la Ujerumani Magharibi STERN liliandika makala mnamo mwaka wa 1974 juu ya "Jesus Starb in Indien", yaani Yesu alifia India.

Gazeti moja la Kijerumani la kila waki HORZU, liliandika mnamo mwaka 1975:

"Fluchtete Jesus nach Indien?" yaani Je Yesu Alikimbilia India? Gazeti hilohilo likatangaza makala mengine katika mwaka huohuo, yaliyosema: Das Gehe i mnis des Grabes von Srinagar, yaani, Siri ya Kaburi la Sri Nagar. Hayo yaliandikwa na Erich' Von Daniken.

Makala mengine yalitangazwa katika gazeti la WEEKEND, London, mwezi wa Julai, mwaka wa 1973. Gazeti la Ghana la kila juma "SPECTATOR" lilitangaza makala katika mwezi wa Machi, 1970 chini ya kichwa cha maneno "Christ Did not Die on the Cross", yaani, Yesu hakufia msalabani.

Nalo gazeti la "SPEAR" la huko Nigeria likiandika katika toleo lake moja la mwaka wa 1977, lilisema: Jesus was Buried in India, yaani Yesu alizikwa huko India.

Ziara hizi zote, na maoni pamoja na makala ni ushuhuda bayana ya kwamba ile sauti iliyotolewa katika kijiji kimoja kidogo miaka 85 iliyopita ilizua mwamsho kote ulimwenguni. Katika majira yale ya mwaka wa 1895, kijiji cha Qadian hakikuwa na barabara za lami, wala njia za reli, wala simu zozote, au vifaa vyovyote vya kuwasiliana na nchi za nje. Na ishara zilizopo zadhihirisha waziwazi ya kuwa mwamko huu waimarika zaidi siku baada ya siku, na kamwe hautakoma mpaka uenee pembe zote za dunia na kila mtu afahamu Umoja halisi wa Mwenyezi Mungu uliohubiriwa na Yesu katika nchi hizi za Himalaya.

KWA NINI KABURI LISIFUKULIWE?

Wazo la kufukuliwa kaburi hilo na kuchunguzwa kisayansi limetolewa zaidi, ya mara moja. Kumesikika uvumi ya kwamba lile kundi lililochunguza majumba ya kale (pyramids) huko Misri kwa kutapanya nuru kali (radiation) ndani ya majumba hayo walikuwa tayari kulichunguza kaburi hilo kwa mbinu hizohizo. Lakini kazi hii yahitaji pesa. Wengine wamependekeza kuchukua picha ya ndani ya kaburi hilo kwa kupenyeza ndani aina fulani ya kamera inayoweza kuzunguka, kuitia shimo lililotobolewa, na kadhalika. Lakini hakuna maendeleo yoyote yaliyofanyika hata hivi sasa.

Hivi sasa ulimwengu umeikodolea macho "Sanda ya Yesu" itakayochunguzwa na halmashauri ya kimataifa mwaka huu (1978). Uchunguzi huu ulioanzishwa mwakawa 1898 waonekana upo karibu kukamilika. Baada ya hapo huenda ulimwengu ukalikodolea macho "Kaburi la Yesu". Ile Sanda ya Yesu ilishughulikiwa na Baraza la Sanda Takatifu la huko Marekani na Tume ya Kimataifa iliyopewa jukumu la kuchunguza Sanda hiyo. Huenda Baraza jingine au Tume maalum vikaanzishwa, kwa minajili ya kutafuta msaada wa ulimwengu mzima ili kuanzisha shughuli za uchunguzi wenyewe manufaa kwa wote.

Kama uchunguzi uliofanyiwa nguo hiyo ya mazishi yenyeye miaka 2,000 umethibitisha ya kwamba Yesu kamwe hakufia msalabani, basi linakuwa jambo lenye kutazamiwa ya kwamba uchunguzi kama huo ufanywe ili kuthibitisha ya kuwa alifia mahali penginepo wakati mwagineo. UMBALI BAINA YA "SANDA YA TURIN" NA "KABURI LA SRI NAGAR" WAWEZA KUWA MREFU, LAKINI UHUSIANO BAINA YA VITU HIVI VIWILI NI WA KARIBU MNO.

BISHARA

Hukumu ya sawa kuhusu kifo cha Yesu na kuzikwa kwake huko Sri Nagar ni hii tu ya kwamba yeze wala hatateremka toka mbinguni, kama wengi wanavyoamini. Kuja kwa Yesu mara ya pili kulitabiriwa, lakini tayari kumetimia barabara katika dhati ya Sayyidna Ahmad a.s. wa Qadian. Yeze asema:

“Kumbukeni ya kwamba hakuna atakayeshuka toka mbinguni. Wapinzani wetu wote waliopo hivi sasa watakuwa na hakuna mmojawapo atakayemuona Yesu mwana wa Mariam akiteremka kutoka mbinguni. Baadaye wazao wao watakaowarithi pia watakuwa bila ya hata mmoja wao atakayemwona Yesu mwana wa Mariam akishuka toka mbinguni. Kadhalika watoto wa wazao wao nao watakuwa bila kumwona mwana wa Mariam akiteremka toka mbinguni. Hapo Mwenyezi Mungu atatia wasiwasi katika nyoyo zao, ya kwamba siku za utukufu wa msalaba tayari zimepita na dunia imeingia katika hatua mpya, ilhali mwana wa Mariam bado hajashuka toka mbinguni. Na hapo wale wenye busara mionganoni mwao wataitupilia mbali imani hii, wote kwa pamoja. NA KUANZIA HII LEO KARNE YA TATU HAITAKUWA IMEPITA ambapo wale wamnganjeo Yesu haidhuru wawe Wakristo au Waislamu, wataudhika mno na kukirihika na kuiacha imani hii mbovu. Na kutabakia na dini moja na kiongozi mmoja tu.

Mimi nimekuja kupanda mbegu. Mbegu tayari nimeipanda kwa mkono wangu. Sasa itamea na kukua na hakuna awezaye kuizua”. *Tazkiratush-shahadatain*, uk. 65, Oktoba, mwaka wa 1903).

(Kitabu hiki kimeandikwa kwa mintarafu ya Mkutano wa Kimataifa kuhusu kunusurika kwa Yesu, utakaofanyika mjini London mwezi Juni, 1978 na kuandaliwa na Jumuiya Waislam Waahmadiyya nchini Uingereza, na utafunguliwa na Khalifa Mtakatifu, Hadhrat Mirza Nasir Ahmad, Mwenyezi Mungu amsaidie).